# Nipashe

Ijumaa Oktoba 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580384

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

www.ippme

nipasheTZ

nipasheTZ

0745 700710

LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500

Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz

Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**MGOMBEA** ubunge wa CHADEMA atiwa matatani

UKURASA 2



**JPM** aongoza kura za awali urais Tanzania

UKURASA 4

UCHAGUZI 2020

UKURASA 2

# Vigogo wabwagwa



Joseph Mbilinyi 'Sugu'



Ester Bulaya



John Heche



Godbless Lema



Joseph Haule 'Prof. J'



Magdalena Sakaya



Mch. Peter Msigwa



Freeman Mbowe



Esther Matiko



Zitto Kabwe

## Lissu, Maalim wanena mazito

UKURASA 3

## Mwinyi kidedea Z'bar

• **CCM** yaibuka mshindi kila kona, yavunja ngome za CHADEMA... *Endelea uk. 2, 18, 19*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



**MICHEZO** **KAZE AFUNGUKA BIASHARA HAICHOMOKI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

UCHAGUZI MKUU 2020

# Vigogo CHADEMA, Zitto wabwagwa

Na Mwandishi wetu

VIGOGO wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambao ni wajumbe wa kamati kuu na wenyeviti wa kanda mbalimbali za chama hicho, wameangushwa vibaya kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba juzi.

Katika kundi hilo la vigogo, yumo pia Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, hivyo kufanya vinara wakongwe wa upinzani waliokuwa wakitamba bungeni kwa miaka 10 na zaidi kufikia 10.

Katika matokeo yaliyotangazwa kwenye majimbo mbalimbali ambayo baadhi yameshikiliwa na upinzani kwa miaka 25, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka na ushindi mkubwa.

Hadi tunakwenda mitamboni, ni jimbo pekee la Mtwara Vijijini ambalo lilitangazwa kwenda upinzani baada ya Hawa Ghasia aliyekuwa mbunge wake kwa miaka 15 kuangushwa. Ghasia alishindwa kwa kupata kura 18,564 dhidi ya Shamsia Mtamba (CUF) aliyeibuka mshindi kwa kupata kura 26,215.

Kwenye majimbo hayo yaliyokuwa chini ya vigogo hao wa upinzani, CCM imeibuka kwa ushindi wa kimbunga ambao haujawahi kutokea tangu Tanzania iingie kwenye mfumo wa vyama vingi.

Viongozi waliobwagwa katika uchaguzi huo ni viongozi wa vyama vya upinzani kwa nafasi tofauti za taifa, akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe wa Hai, Kiongozi Mkuu, Zitto (Kigoma Mjini) na wenyekiti wa kanda.

Jimbo la Moshi Mjini kwa miaka 25 lilikuwa chini ya upinzani kuanzia kwa Philemon Ndesamburo (sasa marehemu) na Jaffary Michael. Sasa kwa mara ya kwanza litaongozwa na mbunge wa CCM.

Katika matokeo hayo, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mbowe, ambaye amekuwa mbunge kwa mwaka 2000, 2010 na 2015, aliangushwa na Saashisha Mafuwe (CCM) aliyepata 89,786 dhidi yake kwa kuambulia kura 27,684.

Mbowe ambaye alikuwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika uchaguzi huo hakupiga kura kutokana na madai ya watu wenye silaha kuvamia nyumbani kwake, kuwapiga walinzi wake na kuondoka nao ambao waliokotwa maeneo ya barabara ya Arusha.

Naye Zitto aliyegombea Kigoma Mjini alipata kura 20,600 huku mshindi akiwa ni Kirumbe Ng'enda aliyepata kura 27,638.

Mwamba mwingine ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi kwa jina maarufu Sugu, aliyekuwa mbunge tangu mwaka 2010. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 alikuwa mbunge pekee aliyepata kura nyingi za ubunge na jimbo lililopiga kura nyingi za urais wa upinzani.

Katika uchaguzi wa juzi, mshindi Jimbo la Mbeya Mjini ni Dk. Tulia Ackson aliyepata kura 75,225 na Sugu alipata kura 37,591. Katika bunge lililopita, Sugu alikuwa Waziri Kivuli wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Dk. Tulia anakuwa mbunge wa kwanza mwanamke kuongoza jimbo hilo tangu kuanzishwa kwake. Mwaka 1995, jimbo hilo liliongozwa na Polisya Mwaiseje wa NCCR- Mageuzi na baadaye kuchukuliwa na Benson Mpesya (CCM) aliyeliongoza kwa miaka 10 tangu mwaka 2020.

Mwamba mwingine ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kusini, Peter Msigwa, ambaye alikuwa Mbunge wa Iringa Mjini kwa miaka 10 kabla ya kubwagwa na Jesca Msambatavangu wa CCM.

Msigwa katika Bunge lililopita alikuwa Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii. Awali, alikuwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa.

Mwingine aliyeangushwa ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Serengeti, Esther Matiko, aliyepata kura 10,873 akiangushwa na Michael Kembaki wa CCM aliyepata kura 18,235.

Aliyekuwa Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, ameangushwa kwa kupata kura 18,757 huku mshindi akiwa ni aliyekuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mwita Waitara aliyepata kura 35,758.

Kigogo mwingine ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Hezekiah Wenje ambaye alikuwa Mbunge wa Nyamagana mwaka 2015 na kuhamia Jimbo la Rorya. Ameangushwa kwa kupata kura 28,168 dhidi ya Jafari Chenge wa CCM aliyepata kura 53,739.

Kigogo mwingine ni Ester Buyala aliyekuwa Mbunge wa Bunda Mjini tangu mwaka 2015. Kabla ya hapo alikuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya CCM. Ameangushwa na Robert Maboto aliyepata kura 31,129 huku akiambulia kura 13,258.

Katika Bunge lililopita Bulaya alikuwa Waziri Kivuli (Ofisi ya Waziri Mkuu) Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini kwa miaka 10 mfululizo, Godbless Lema (CHADEMA), ameanguka baada ya kupata kura 46,489 dhidi ya 82,480 za Mrisho Gambo wa CCM aliyetangazwa mshindi jana.



Aliyekuwa mgombea udiwani Kata ya Nzuguni, jijini Dodoma jana, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godfrey Chipungu, akiangua kilio baada ya matokeo kutangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Kata hiyo, Hamisi Jingwa (hayupo pichani), kuwa ameshindwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mgombea mbaroni tuhuma kumpiga mateke msimamizi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limemkamata na kumshikilia Mgombea wa Ubunge wa Shinyanga Mjini, Salome Makamba (CHADEMA) kwa tuhuma za kumshambulia kwa kumpiga mateke msimamizi wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi usiku na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, tukio hilo linadaiwa kutokea juzi majira ya saa mbili usiku, Makamba alipoomba kuona matokeo na baada ya kutoridhika nayo, aliyachana na kuanza kumshambulia msimamizi huyo wa uchaguzi akiwa na wafuasi wake.

Alisema baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi lilimsaka na kumkata na kumweka mahabusu na upelelezi ukikamilika, atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili.

"Mgombea huyu ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia CHADEMA, tunamshikilia kwa kosa la kufanya fujo na kumjeruhi msimamizi wa uchaguzi katika Kituo cha Ugweto B aitwaye Farida John kwa kumpiga ngumi na mateke," alisema Magiligimba. Alitoa wito kwa wagombea pamoja na wafuasi wa vyama mbalimbali, kuacha kufanya fujo ambazo zitahatarisha uvunjifu wa amani, bali waridhike na matokeo.

# Dk. Mwinyi kidedea urais Zanzibar

Na Waandishi Wetu

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Huseein Ali Mwinyi, ametangazwa mshindi wa nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika juzi. Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo jana, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Mstaafu Himid Mahmoud, alisema Dk. Mwinyi ameibuka na ushindi kwa kupata kura 380,402 sawa na asilimia 76.27 ya kura halali zilizopigwa.

Katika matokeo hayo, mgombea wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 99,103 sawa na asilimia 19.87 ya kura zote. Jumla ya wagombea 17 walijitokeza kuwania nafasi hiyo.

Jaji Himid alisema katika uchaguzi huo, wananchi wa Zanzibar 566,352 walijiandikisha kupiga kura, lakini waliojitokeza walikuwa 498,786 ambao ni sawa na asilimia 88.07 ya wapigakura wote.

"Kwa mujibu wa kifungu 96 (2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Na. 4 ya mwaka 2018, namtangaza Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Chama Cha Mapinduzi kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais wa Zanzibar uliofanyika Oktoba 28, 2020," alisema Jaji Himid.

Kwa matokeo hayo, Dk. Mwinyi ambaye ni Rais Mteule wa Zanzibar, anatarajiwa kuwa Rais wa awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu kuasisiwa kwa Mapinduzi ya Zanzibar.

Marais wengine waliomtangulia ni Sheikh Abeid Amani Karume (1964- 1972), Alhaji Aboud Jumbe (1972-1984), Ali Hassan Mwinyi (1985-85), Idris Abdul Wakil (1985-1990), Dk. Salmin Amour Juma (1990- 2000), Amani Abeid Karume (2000- 2010) na Dk. Ali Mohamed Shein (2010- 2020).

**MWENYEWE ATOA NENO**

Akizungumza baada ya kutangazwa na kukabidhiwa cheti cha ushindi, Dk. Mwinyi aliwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kutumia haki yao ya kikatiba kuchagua viongozi, kipekee kumchagua kuwa Rais mpya wa visiwa hivyo.

"Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua hii ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa urais wa Zanzibar. Nimepokea na kuyakubali matokeo ya uchaguzi wa Oktoba 28. Pia nimepokea kwa moyo na kwa mikono miwili uamuzi wa wananchi wa Zanzibar walioamua mimi Hussein Mwinyi kuwa rais wa awamu ya nane," alisema.

Pia Dk. Mwinyi aliwataka wagombea wote waliochuana naye kuungana kwa pamoja na kuijenga Zanzibar bila kujali tofauti zao, huku akiahidi kuendeleza maridhiano yaliyomo katika Katiba ya Zanzibar. "Zanzibar ni kubwa kuliko tofauti zetu. Nawaomba wote tuungane kwa pamoja na kuendeleza umoja, amani na mshikamano kwa manufaa ya Zanzibar. Tuponye madonda ya uchaguzi sasa tuijenge Zanzibar mpya.

Katika hatua nyingine aliwashukuru wana CCM kwa kumpitisha kuwa mgombea urais na hatimaye kumchagua kuwa Rais kwa kura za kishindo.

"Mimi si bora kuliko CCM. Ushindi huu ni wa wana CCM wote. CCM ina wanachama wenye uwezo kuliko mimi lakini mlinichagua mimi kuwa mgombea. Imani mliyoionyesha kwangu ni kubwa. Imani huzaa imani, hivyo nitawalipa imani kwa utumishi uliotukuka," alisema.



Mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akidai kuwa uchaguzi mkuu umevurugwa na haukuwa na usawa. Kushoto ni mgombea mwenza wake, Salum Mwalimu na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tundu Lissu: Siyatambui matokeo Uchaguzi Mkuu

**Na Beatrice Shayo**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ametangaza kutoyatambua matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika, Oktoba 28, kwa madai ya kuwapo kwa ukiukwaji wa kidemokrasia ikiwamo kuzuiwa mawakala wao kinyume cha sheria za uchaguzi.

Kadhalika, ametoa wito kwa Jumuiya za Kimataifa zilizokuja nchini kwa ajili ya uangalizi wa uchaguzi kueleza ukweli kwa kile kilichotokea, ili hatua zichukuliwe kwa waliohusika kwa kuharibu uchaguzi huo.

Lissu alitoa msimamo huo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa kilichofanyika Oktoba 28, mwaka huu, haukuwa uchaguzi kutokana na ukiukwaji mkubwa uliofanywa.

"Hapakuwa na uchaguzi wenye viwango vya uchaguzi unaotakiwa...huu sio uchaguzi, wamefanya uharamia," alidai Lissu.

Kadhalika, alisema kwa mujibu wa sheria za Tanzania na za kimataifa za uchaguzi, inataka kuwapo na mawakala jambo ambalo lilizuiliwa kwa mawakala wao.

"Mawakala wetu wamezuiliwa kuingia licha ya majina yao kuwapo na wengine kutolewa kwa nguvu kwenye vituo vya kura kinyume cha sheria za uchaguzi," alisema Lissu.

Alisema sheria inasema wakala ana haki ya kupata nakala ya matokea katika kituo alichosimamia, jambo ambalo alidai halikufanyika.

Kadhalika, alidai kuna baadhi ya maeneo ziliingizwa kura feki likiwamo Jimbo la Kawe, jijini Dar es Salaam.

Alidai wamekamata kura feki ambazo zilipigwa kwa mgombea wa urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli na kwa mgombea ubunge wa Jimbo la Kawe (CCM), Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Msigwa.

"Kata nzima CCM inatangazwa ni washindi inawezekanaje kwenye uchaguzi huu ambao ulikuwa na ushindani mkubwa kuliko chaguzi nyingine, hii haiwezekani kila maeneo washinde wao CCM," alisema.

Vile vile, Lissu alidai kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi ngazi ya urais ni uharamia kwa sababu suala hilo hutumia muda walau siku mbili na kuendelea kutokana na mchakato uliopo wa upokeaji wa matokea kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa mrefu.

Alidai Watanzania waliokwenda kupiga kura wamefanyiwa uhuni japo ni haki yao ya kimsingi kumchagua kiongozi wanayemtaka.

"Watanzania wawe tayari kudai demokrasia sio kuwa na viongozi wanaowataka wao badala ya wale ambao wamechaguliwa na wananchi," alisisitiza.

Kuhusu Jumuiya ya Kimataifa, alisema Taasisi za Kimataifa, Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki na walioleta watazamaji, zisitoe matangazo kama kulikuwa na uchaguzi badala yake waeleze taarifa za kweli kilichotokea katika uchaguzi mkuu.

Akifafanua, alisema yeyote kama ni Tume ama ni vyombo vya usalama vimehusika kuharibu uchaguzi huo wachukuliwe hatua kwa mujibu wa taratibu za kimataifa.


## PASSPORT IMEPOTEA



**ROSE MBAULIDIA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE010604** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2018. Ilipotea tarehe 02/09/2020 Maktaba Kuu DSM. Tukio hili limeripotiwa katika kituo cha Polisi Msimbazi na kupewa Kumb: **DAR/MSI/RB/642288/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu au awasiliane kwa simu Na. **0719 436813.**


# Maalim Seif atangaza maandamano kudai haki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amekataa kutambua zoezi zima la uchaguzi mkuu na kutangaza rasmi kudai haki kwa njia ya maandamano ya muda usiojulikana.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, Vuga mjini hapa kabla ya matokeo ya urais kutangazwa, alisema uchaguzi mkuu wa Zanzibar umevurugwa.

Maalim Seif alisema njama za kuvuruga uchaguzi zimeanza kujitokeza katika uchaguzi wa kura ya mapema, Oktoba 27 kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, ikiwamo kufukuzwa kwa mawakala wa chama chao kila walipokuwa wakihoji au kuzuiwa kufanyika vitendo vya kuvuruga uchaguzi.

"Mawakala wetu wamenyimwa orodha ya madaftari ya wapigakura na kila walipohoji kwanini watu wanapiga kura zaidi ya moja walitolewa nje ya kituo kwa madai ya kwamba wanafanya fujo," alisema Maalim.

Alidai matokeo yote yaliotangazwa ya Uwakilishi, Ubunge na Udiwani ni ya kupikwa yaliyopangwa na Tume ili kuhakikisha CCM inabaki madarakani.

"Tumeamua kudai haki kwa njia ya maandamano baada ya haki yetu kupitia njia ya demokrasia kushindikana, nawaomba wananchi tukutane Michenzani kwa ajili ya maandamano," alisema.

Baada ya mkutano wake na waandishi wa habari, viongozi wa chama hicho na watendaji wote waliokuwa katika ofisi hizo walianza kuondoka kuelekea Michenzani na baada ya nusu saa milio na mabomu ilianza kusikika katika mitaa ya Darajani na Michenzani huku wapitanjia wakionekana kukimbizana barabarani kwa kuhofia usalama wao.


TANZANIA MENTORS ACTION TMA

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE YEAR 2020/2021

**A. Background.**

**Tanzanian Mentors Action (TMA)** is a Non-Governmental Organization (NGO) established in May 2013 by Mentors who were previously employed as consultants to implement WAJIBIKA project. WAJIBIKA project was three years USAID funded project with a purpose of strengthening programmatic and fiscal accountability in the Government including Local Government Authorities. It was established in May 2013 with registration no 99555. The organization is also officially registered with Tanzania Revenue Authority (TRA) with TIN No: 122-910-938. Currently TMA is implementing USAID and DFID projects to strengthen Publics systems across 5 components namely information system, Governance, Finance, Human Resources and Monitoring and Evaluation and learning in all regions and Local Government Authorities of Tanzania.

TMA office is now inviting applications from eligible, competent, and qualified Companies to apply for pre-qualification for provision of Goods and Services for its operations in Tanzania as indicated below.

| LOT NO | DESCRIPTION OF SERVICES |
|---|---|
| 1 | Stationeries |
| 2 | Publication and Printing |
| 3 | Insurance (Medical, life, Vehicle, Assets) |
| 4 | Internet Service Provider |
| 5 | Security Services |
| 6 | Office Repair and Maintenance(Plumbing, carpentry, printer maintenance) |
| 7 | Food and refreshments supply |
| 8 | Fleet Management System (Car GPS and tracking) |
| 9 | Car rentals |
| 10 | Generator maintenance |
| 11 | General Cleaning Company |
| 12 | Authorize Dealers (HP/DELL and LENOVO) |
| 13 | Event Planning and Decorations |
| 14 | Legal Services |
| 15 | Travel Agents |
| 16 | Auditing Services |

| | |
|---|---|
| 17 | Media Houses |
| 18 | Conference Packages (Meetings/trainings/ workshop) |
| 19 | Supermarkets |
| 20 | ICT Equipment's & Services |
| 21 | Office Furniture's Fittings |
| 22 | Vehicle Maintenance/Tires |
| 23 | Fuel |
| 24 | ConsultancyServices: |
| | I. Research, Monitoring, Evaluation,Result Bases Management and Management Information System.<br>II. Accounting, Procurement and Process Management system (Software Developer/ Vendor). |
| 25 | Tax advice services |
| 26 | Transportation services |
| 27 | Accommodation services |

**The purpose of this Expression ofInterest:**

3. Is to identify suppliers with verified technical and financial capacity to provide the goods or perform the services. Eligible suppliers will be invited to participate in the bidding process for theproposed tender.

4. Eligibility to participate in the proposed tender will be determined based on the following:
   - The supplier must have legal capacity to enter into a contract
   - Must have proven financial capacity in their line of business for 2 years: (Latest audited financial statements).
   - The products or service offered must be of interest to TMA and supplier must have the necessary and professional and technical competence.
   - After the deadline for submission of responses has passed, TMA will evaluate responses receivedand will notify eligible participants of the outcome of the evaluation.

**C. How to prepare and submit your expression of Interest.**
- TMA is hereby invites qualified supplier to express their interest by emailing to procurement@tma.or.tz with the subject of the description of service you are interested with.
- The deadline for response to this Expression of Interest is 15stNovember 2020
- In order to participate in the pre-qualification exercise, companies are required to provide thefollowing:

| | |
|---|---|
| • Copy of Company Profile | Copy of Business License |
| • Copy of Tax Identification Number(TIN) | Copy of Tax Clearance certificate. |
| • Copy of Tax VAT Registration Number (VRN) | |
| • Copy of Certificate of Incorporation | |
| • Company Annual audited financial report of the last two years(2) | |
| • Copy of Certificate of Registration | |

- TMA will not consider incomplete submission. All responses and supporting documentation willbe treated as strictly confidential and will not be made available to the public.
- Should you have any question please do not hesitate to contact us at **procurement@tma.or.tz**

# JPM aongoza matokeo urais

Na Mwandishi Wetu

MGOMBEA Urais wa Tanzania kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, anaongoza katika matokeo ya urais katika majimbo yaliyoanza kutangazwa jana.

Katika matokeo hayo yanayoendelea kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Magufuli ambaye anawania muhula mwingine kuongoza nchi, anaongoza kwa asilimia kati ya 70 na 95 akifuatiwa kwa mbali na mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, wagombea wengine waliojitosa katika kinyang'anyiro hicho, akiwamo Bernard Membe wa ACT-Wazalendo, na Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), wanaambulia chini ya wastani wa asilimia moja ya kura zilizopigwa.

**Matokeo hayo ni kama ifuatavyo;-**

**KONDOA MJINI**

Dk. Magufuli (15,616) Leopard Mahona (NRA) kura 13, John Shibuda (ADA TADEA) kura 35, Muttamwega Mgahywa (SAU) 14, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 38, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 20, Lipumba (187), Philipo Fumbo (DP) tisa, Membe (9) na Queen Sendiga (ADC) kura tano.

Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) nne, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 30, Khalfan Mazrui (UMD) moja, Seif Seif (AAFP) mbili na Lissu kura 1,596.

**SIHA**

Magufuli (26,056), Lissu (5,124), Mahona (119), Shibuda (74), Muttamwega (23), Mwanga (32), Maganja (17), Lipumba (14), Fumbo (17), Membe (11), Sendiga (7), Kadege (21), Rungwe (133), Mazrui (5) na Seif (4).

**NKENGE**

Dk. Magufuli (57,975), Lissu (5,145), Mahona (222), Shibuda (93), Muttamwega (44), Mwanga (42), Maganja (80), Lipumba (101), Fumbo (22), Membe (33), Sendiga (15), Kadege (12), Rungwe (117), Mazrui (3) na Seif (7).

**LUPEMBE**

Magufuli (27,527), Lissu (1,286), Mahona (127), Shibuda (61), Muttamwega (33), Mwanga (20), Maganja (25), Lipumba (8), Fumbo (16), Membe (120, Sendiga (11), Kadege (7), Rungwe (30), Mazrui (3) na Seif (4).

**SHINYANGA MJINI**

Magufuli (38,411), Lissu (10,597), Mahona (222), Shibuda (103), Muttamwega (33), Mwanga (45), Maganja (57), Lipumba (42), Fumbo (17), Membe (62), Sendiga (11), Kadege (8), Rungwe (220), Mazrui (6) na Seif (4).

**IRAMBA MASHARIKI**

Dk. Magufuli (37,231, Lissu (4,273), Mahona (391), Shibuda (121), Muttamwega (61), Mwanga (36), Maganja (75), Lipumba (41), Fumbo (23), Membe (26), Sendiga (11), Kadege (14), Rungwe (73), Mazrui (5) na Seif (13).

**MAKAMBAKO**

Magufuli (23,000), Mahona (98), Shibuda (43), Muttamwega (12), Mwanga (27), Maganja (12), Lipumba (11), Fumbo (10), Membe (14), Sendiga (7), Kadege (4), Rungwe (39), Mazrui (3), Seif (8) na Lissu (4,840).

**ILEJE**

Magufuli (30,373), Mahona (317), Shibuda (106), Muttamwega (29), Mwanga (56), Maganja (12), Lipumba (10), Fumbo (25), Membe (12), Sendiga (12), Kadege (16), Rungwe (70), Mazrui (4), Seif (12) na Lissu (5,372).

**NJOMBE MJINI**

Magufuli (30,134), Mahona (138), Shibuda (62), Muttamwega (10), Mwanga (39), Maganja (38), Lipumba (6), Fumbo (19), Membe (13), Sendiga (14), Kadege (9), Rungwe (45), Mazrui (3) , Seif (6) na Lissu (5,138).

**MAFINGA MJINI**

Magufuli (17,117), Mahona (60), Shibuda (33), Muttamwega (7), Mwanga (12), Maganja (18), Lipumba (15), Fumbo (6), Membe (8), Sendiga (6), Kadege 12), Rungwe (31), Mazrui (3), Seif (2) na Lissu (2,673).

**MAKUNDUCHI**

Dk. Magufuli (9,774), Mahona (37), Shibuda (13), Muttamwega (21), Mwanga (10), Maganja (15), Lipumba (76), Fumbo (7), Membe (443), Sendiga (51), Kadege (19), Rungwe (49), Mazrui (9), Seif (8) na Lissu (718).

**BUSEGA**

Magufuli (37,565) Mahona (692), Shibuda (249), Muttamwega (90), Mwanga (52), Maganja (72), Lipumba (61), Fumbo (37), Membe (75), Sendiga (23), Kadege (35), Rungwe (98), Mazrui (10), Seif (22) na Lissu (7,512).

**BUNDA**

Magufuli (16,008), Mahona (257), Shibuda (73), Muttamwega (30), Mwanga (29), Maganja (46), Lipumba (17), Fumbo (15), Membe (20), Sendiga (3), Kadege (13), Rungwe (62), Mazrui (10), Seif (3) na Lissu (3,500).

**HANANG'**

Magufuli (61,041), Mahona (514), Shibuda (186), Muttamwega (59), Mwanga (65), Maganja (67), (57), Fumbo (26), Membe (76), Sendiga (19), Kadege (34), Rungwe (134), Mazrui (10), Seif (23) na Lissu (11,141).

**MWANAKWEREKWE**

Magufuli (9,252), Mahona (33), Shibuda (23), Muttamwega (15), Mwanga (5), Maganja (31), Lipumba (63), Fumbo (8), Membe (1,320), Sendiga (39), Kadege (12), Rungwe (76), Mazrui (6), Seif (4) na Lissu (2,135).

**MBEYA MJINI**

Dk. Magufuli (77,562), Mahona (501), Shibuda (227), Muttamwega (46), Mwanga (139), Maganja (97), Lipumba (85), Fumbo (23), Membe (76), na Sendiga (20), Kadege (26), Rungwe (394), Mazrui (5), Seif (6) na Lissu (34,287).

**CHUMBE**

Magufuli (1,952), Mahona (144), Shibuda (55), Muttamwega (51), Mwanga (39), Maganja (25), Lipumba (63), Fumbo (12), Membe (676), Sendiga (50), Kadege (16), Rungwe (40), Mazrui (13), Seif (19) na Lissu (991).

**MADABA**

Magufuli (12,450), Mahona (67), Shibuda (39), Muttamwega (6), Mwanga (12), Maganja (28), Lipumba (18), Fumbo (4), Membe (11), Sendiga (7), Kadege (2), Rungwe (17), Mazrui (1), Seif (2) na Lissu (1,267).


## Equity Bank (Tanzania) Limited (UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

EQUITY Bank • Your Listening, Caring Partner

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE : 30 SEPTEMBA 2020

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-20 | Robo Mwaka ya 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 21,191 | 23,962 |
| 2. | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 26,387 | 38,106 |
| 3. | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 113,796 | 86,042 |
| 4. | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 45,652 | 86,087 |
| 5. | Hundi na Miamala ya Kushugulikiwa | - | - |
| 6. | Miamala Isiyoshugulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 7. | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. | Mikopo iliyotolewa na Benki nyingine | 33,980 | 34,540 |
| 10. | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. | Mikopo Halisi Iliyopo | 287,213 | 284,308 |
| 12. | Mali Nyingine | 30,097 | 30,988 |
| 13. | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 11,087 | 11,371 |
| 16 | Haki ya mali | 11,964 | 11,964 |
| **17.** | **JUMLA YA MALI** | **581,367** | **607,368** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 18. | Amana za Benki na Taasisi za Fedha | - | 1,448 |
| 19. | Amana za Wateja | 356,149 | 378,658 |
| 20. | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 21. | Amana Maalumu | 864 | 1,924 |
| 22. | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 23. | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 41 | 40 |
| 24. | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,456 | 2,778 |
| 25. | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 26. | Miamala Isiyoshugulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 27. | Mapato yalioingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 2,299 | 2,017 |
| 28. | Dhima Nyingine | 6,556 | 8,900 |
| 29 | Dhima ya kukodisha | 7,641 | 7,641 |
| 30. | Madeni | 99,287 | 97,177 |
| **31.** | **JUMLA YA DHIMA** | **476,293** | **500,583** |
| **32.** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **105,075** | **106,785** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 33. | Mtaji wa Hisa Uliolipiwa | 125,218 | 125,218 |
| 34. | Akiba ya Mtaji | 400 | 400 |
| 35. | Mapato yaliyobakizwa | (32,744) | (32,744) |
| 36. | Faida(Hasara) ya Kipindi Husika | (5,385) | (3,675) |
| 37. | Akaunti Nyingine za Mtaji | 17,587 | 17,587 |
| 38. | Stahiki ya Wenye hisa Chache | - | - |
| **37.** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **105,075** | **106,785** |
| 38. | Dhima Zisizo Dhahiri | 199,405 | 197,024 |
| 39. | Mikopo Chechefu | 136,543 | 147,842 |
| 40. | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 74,444 | 67,748 |
| 41. | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I). | Uwiano wa fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 18.07% | 17.58% |
| (ii). | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 38.18% | 42.24% |
| (iii). | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 104.16% | 94.18% |
| (iv). | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 49.40% | 46.81% |
| (v). | Uwiano na Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 74.82% | 66.70% |
| (vi). | Ongezeko la Amana | -6.55% | 5.91% |
| (vii). | Ongezeko la Mali | -4.28% | 11.89% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-20 | Robo Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 18,019 | 11,458 | 40,747 | 38,121 |
| 2. Gharama za Riba | (6,149) | (6,471) | (19,180) | (18,276) |
| **3. Mapato Halisi ya Riba** *(1 kutoa 2)* | **11,871** | **4,987** | **21,567** | **19,845** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Hasara Katika Mikopo | 10,140 | - | 14,561 | - |
| **6. Mapato Yasiyo ya Riba:** | **5,300** | **3,344** | **13,630** | **11,742** |
| 6.1 Faida/(Hasara) Zitokananazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2,623 | 1,112 | 5,742 | 3,842 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 2,335 | 2,225 | 6,980 | 7,881 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 343 | 7 | 908 | 20 |
| **7. Gharama Zisizo na Riba:** | **(8,741)** | **(11,483)** | **(26,270)** | **(29,182)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,326) | (3,605) | (9,900) | (10,819) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (1,006) | (1,058) | (3,213) | (4,919) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (4,409) | (6,819) | (13,157) | (13,444) |
| **8. Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,710)** | **(3,152)** | **(5,634)** | **2,406** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 945 | 249 | (722) |
| **10. Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,710)** | **(2,206)** | **(5,385)** | **1,684** |
| **11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisha)** | 0 | (136) | 1,289 | (210) |
| **12. Jumla ya Faida(Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,710)** | **(2,342)** | **(4,097)** | **1,474** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 399 | 407 | 399 | 407 |
| 14. Mapato kwa Hisa | - | - | - | - |
| **15. Idadi ya Matawi** | **14** | **14** | **14** | **14** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | -1.2% | -2.2% | -1.3% | 0.6% |
| (II) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -8.4% | -14.9% | -8.8% | 3.8% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 50.9% | 137.8% | 74.6% | 92.4% |
| (iV) Uwiano Wa Mapato halisi ya riba na wastani wa mali zinazo zalisha | 11.5% | 4.9% | 7.0% | 6.5% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-20 | Robo/ Mwaka Uliopita Tarehe 30-Juni-2020 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shuguli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato / (Hasara) Halisi | (1,959) | (2,101) | (5,634) | 2,406 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 9,819 | 6,342 | 18,355 | 3,616 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (13,046) | 4,168 | (4,172) | 30,613 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (25,016) | 33,738 | (3,686) | 997 |
| | - Mabadiliko katika dhamana ya muda mfupi | (27,753) | (14,978) | (48,329) | (7,238) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 797 | (1,068) | 1,906 | 3,239 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (4,048) | 3,549 | 2,296 | (11,492) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | (3,443) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 3,631 | 689.02 | 7,268 | 1,117 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shuguli za Uendeshaji* | **(57,576)** | **30,339** | **(31,994)** | **19,813** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shuguli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopekewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (855) | (575) | (1,480) | (2,194) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo(Bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shuguli za Uwekezaji* | **(855)** | **(575)** | **(1,480)** | **(2,194)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shuguli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (6,445) | (6,445) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | 51,705 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (719) | (1,586) | (2,305) | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shuguli za Kifedha* | **(719)** | **(8,030)** | **42,955** | **-** |
| **IV** | **Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali | **(59,151)** | **21,734** | **9,481** | **17,620** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni | **165,291** | **143,556** | **96,659** | **118,594** |
| | *Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka* | **106,140** | **165,291** | **106,140** | **136,213** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa (2020)** | 73,513 | 400 | (32,744) | 15,463 | - | 835 | 57,466 |
| Ongezeko la Mtaji | 51,705 | - | - | - | - | - | **51,705** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (5,385) | - | - | - | **(5,385)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 1,289 | **1,289** |
| Miamala ya wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililopita | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada la Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio 30 Septemba 2019** | **125,218** | **400** | **(38,129)** | **15,463** | **-** | **2,124** | **105,075** |

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka Uliopita (2019)** | 73,513 | 400 | (17,170) | - | 2,498 | 719 | **59,960** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (2,609) | - | - | | **(2,609)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (15,463) | 15,463 | - | - | - |
| Tengo la Ziada la Jumla | - | - | 2,498 | - | (2,498) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 116 | **116** |
| **Salio 31 Desemba 2019** | **73,513** | **400** | **(32,744)** | **15,463** | **-** | **835** | **57,466** |

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|
| Robert Kiboti **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **imesainiwa** | **27.10.2020** |
| George Radonde **(Mkuu wa Fedha)** | **imesainiwa** | **27.10.2020** |
| Douglas Bashobeza **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani )** | **imesainiwa** | **27.10.2020** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|
| Raymond Mbilinyi **(Mweyekiti wa Bodi)** | **imesainiwa** | **27.10.2020** |
| Prof. Ahmed Ame **(Mkurugenzi )** | **imesainiwa** | **27.10.2020** |

Benki iliadhibiwa TZS 8m na BOT kwa kutofuata Kanuni ya Fedha za Kigeni

# Aangua kilio kushindwa kwa kura 67

**Na Ibrahm Joseph,** DODOMA

MGOMBEA udiwani Kata ya Nzuguni kupitia CHADEMA, Godfrey Chipungu, amejikuta akiangua kilio mbele ya wapigakura akiwa haamini matokeo ya uchaguzi huo kutangazwa kuwa mgombea wa CCM ameshinda.

Kwa mujibu wa karatasi iliyobandikwa na msimamizi wa uchaguzi kata hiyo, Hamisi Jigwa, Chipungu alipata kura 1,958, huku mgombea wa CCM, Aloyce Luhega, akipata kura 2,025.

Baada ya kuona matokeo hayo, Chipungu aliangua kilio mbele ya wananchi waliojitokeza kudai matokeo ambayo walidai kuwa yamechelewa kutangazwa hadi jana asubuhi.

Akieleza sababu za kuangua kilio hicho mbele ya wananchi, Chipungu, alidai kuwa matokeo yaliyobadikwa kwenye vituo yalionyesha kuwa yeye alishinda, hivyo aliamini amehujumiwa.

Hata hivyo, aliwaomba wakazi wa kata hiyo waliojitokeza kutofanya fujo wasubiri mpaka atakapowasiliana na viongozi wake wajue watakachofanya.

Wananchi wa kata hiyo walikusanyika nje ya ofisi ya mtendaji wa kata kudai matokeo yalivocheleweshwa kutokana na kurudiwa kuhesabiwa kura.

Msimamizi wa uchaguzi wa kata, Hamisi Jigwa, alilazimika kubandika matokeo akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi kutokana na kuhofia kushambuliwa na wananchi waliojitokeza kudai kuwa mgombea wa CHADEMA alikuwa ameshinda.

# Waangalizi ndani waridhishwa uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANGALIZI wa ndani wa uchaguzi kupitia Jumuiya ya Wanawake wenye ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), wamesema wameridhishwa na mwenendo wa uchaguzi mkuu uliofanyika juzi.

Msimamizi wa Mipango wa JUWAUZA, Salma Hairawa Saadat, aliyasema vituo vya kupigia kura vilifunguliwa kwa wakati na vifaa vya kupigia kura vilitosheleza.

Alisema kuwa waangalizi hao walibaini kuwa upigaji kura ulifanyika kwa faragha na utulivu mkubwa tofauti na hali iliyokuwapo Oktoba 27 katika kura ya mapema na askari kulazimika kutumia mabomu ya machozi.

"Hali ilikuwa shwari na watu wengi walijitokeza kupiga kura pamoja na kuwapo kwa hali ya mvua," alisema.

Alisema kulijitokeza baadhi ya changamoto kwa watu wenye ulemavu waliopewa vitambulisho maalum na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ili kuwawezesha kupata msaada na kupiga kura.

"Watu wenye ulemavu walifika katika vituo mapema ila kulijitokeza changamoto ya polisi kuwazuia kwa madai kuwa hawavitambui vitambulisho hivyo," alisema. Vile vile, alisema kumejitokeza tatizo lingine la kutofikiwa kwa urahisi baadhi ya vituo kwa watu wenye ulemavu wa viungo kupanda vidaraja katika vituo.

Aidha, alisema kumekuwapo kwa changamoto zilizotokea wakati wa kupiga kura hasa kwa watu wenye ulemavu wasioona ambao wengi hawakupata kusaidiwa kwa sababu wasaidizi wa Tume hawakuzifahamu nukta nundu.

Alisema asilimia 90 ya waangalizi wa jumuiya hiyo, waliokuwapo katika vituo vyote vya Unguja na Pemba walishuhudia uwepo wa kura za mapema zilizopigwa Oktoba 27, ambazo zilikuwa katika bahasha na kutumbukizwa katika masanduku ya kupiga kura kabla ya wapigakura kuanza kupiga kura.

Alibainisha waangalizi hao walibaini kuwapo kwa baadhi ya wapigakura ambao majina yao yalikosekana katika daftari la wapigakura, na hawakuweza kupiga kura.


EQUITY Bank • Your Listening, Caring Partner

## EQUITY BANK TANZANIA LIMITED TARIFF GUIDE

| SERVICE | CURRENCY | |
|---|---|---|
| **Account Opening Balance** | **TZS** | **OTHER CURENCIES-AMOUNT IN USD EQUIVALENT USD, EURO,GBP& KES** |
| Personal Account | 20,000 | 100 |
| Personal Account - Supreme Branch | 2,000,000 | 2,000 |
| Business Account - Supreme Branch | 10,000,000 | 5,000 |
| Business Account | 10,0000 | 200 |
| Malezi Member | 10,000 | n/a |
| Jijenge Account | 10,000 | n/a |
| Teeniz Account | 10,000 | n/a |
| Achievers Student Account | 10,000 | n/a |
| Elimika Account | 10,000 | n/a |
| **Minimum Balance Requirements** | | |
| Personal Account | nil | 100 |
| Business account | nil | 100 |
| Supreme Branch | nil | 100 |
| **Fixed Deposit Account/Akaunti ya Muda Maalum** | | |
| Fixed Deposit Account Minimum Balance | 1,000,000 | 1,000 |
| Fixed deposit withdrawal on maturity | nil | nil |
| Fixed deposit premature withdrawal | Loose 5 0 % of accrued interest | |
| **Account Closing Charges** | | |
| Account closure fee | 15,000 | TZS Equivalent |
| **Cash Withdraw over the counter** | | |
| Retail - Over the Counter Cash withdrawal | 2,500 | 0.01 |
| Corporate over the Counter Cash withdrawal | 3,000 | TZS Equivalent |
| Non corporate customers being served at corporate section | 3,000 | TZS Equivalent |
| Charges below minimum balance | nil | 10 |
| Cash handling fee | Free | free |
| Inter-Branch Cash Withdrawal | 3,000 | 0.50% |
| Bulk cash withdrawal over 50 Million | 0.05% | TZS Equivalent |
| **Bulk Cash Counting/Deposit Of small Denominations** | | |
| Bulk Cash deposit notes over 5,000,000 (Tzs denomination fromTZS 2,000 and below) | 0.50% | USD denomination 20,10,5,2,1 0.25% |
| Bulk cash deposit coins over TZS 10,000/= | 0.50% | n/a |
| InterBranch Cash Deposit | Free | Free |
| **Cheque and Bankers Cheque** | | |
| Cheque Books - Small (Inclusive 2.5 Stamp Duty) | 500 per leaf | USD 0.25 |
| Cheque Books - Large (Inclusive 2.50 Stamp Duty) | 500 per leaf | USD 0.25 |
| Counter Cheque (Current Account Withdrawal Without Cheque Leave) | 7,500 | 5 |
| Bankers Cheques - Customers | 10,000 | (Foreign Draft) 20 |
| Bankers Cheques - Non- Customers | 10,000 | (Foreign Draft) 20 |
| Cheque Stop Payment instructions | 20,000 | 10 |
| Unpaid Cheque - RD/ENC (inwards) | 60,000 | 30 |
| Unpaid Cheque - Technical reasons (inwards) | 40,000 | 20 |
| Unpaid Cheque (outwards) | 15,000 | 15 |
| Foreign Cheques for collection | n/a | 0.1% min $40 |
| Travellers cheques collection charges | n/a | 15 |
| Courier charges FCY cheques | n/a | 40 |
| Cash & Cheque Deposit Books | 5,000 | TZS Equivalent |
| Transaction fees - Inward Clearing | 1,500 | TZS Equivalent |
| Transaction fees - Outward Clearing | Free | Free |
| **Funds Transfer** | | |
| Internal funds transfer(same branch and currency) | 2,500 | TZS Equivalent |
| Transfer From FCY to LCY and vise versa | Free | Free |
| Standing Orders/EFTs - Internal | Free | Free |
| External salary remitance /eft | 3,000 | Nil |
| Standing Orders/EFTs - External (remitting) | 3,000 | Nil |
| Standing Orders/EFTs - unpaid (remitting) | 13,000 | TZS Equivalent |
| standing order amendments | 10,000 | TZS Equivalent |
| TISS Incoming | free | free |
| TISS Outgoing(CHARGES) | 11,800 | TZS Equivalent |
| Outgoing Foreign Remittance -SWIFT ( customer) | n/a | 50 |
| Incoming Swift foreign remittance | n/a | 10 |
| East African Payments with East African community countries (in their local currencies) | 11,800 | TZS Equivalent |
| **Other Transactions Fees & Charges** | | |
| Cash handling fee | Free | free |
| Ledger Fees | Nil | Nil |
| Search fees | 50,000 | TZS Equivalent |
| Remittances - Salaries | 2,000 | TZS Equivalent |
| Postage | 1,500 | TZS Equivalent |
| Interim Statement | 2,000 per page | 1 US $ per page |
| Bank Opinion/Introduction/Credit Reference | 40,000 | TZS Equivalent |
| Interest certificate (free for churches) | 10,000 | TZS Equivalent |
| Certification of Balances for Audit purposes | 40,000 | TZS Equivalent |
| Inter company transactions ( deposit/withdrawal) in local currency | Free | Free |
| Inter company transactions ( deposit/withdrawal) in foreign currency | 1% - min $10 max $100 | 1% - min $10 max $100 |
| Registered Mail postage | 6,500 | TZS Equivalent |
| Retrieval of documents >1 month old 15,000 and above one year | 30,000 | TZS Equivalent |
| PAYE Remittances | 10,000 per remittance | TZS Equivalent |
| Photo copy per page | 2,000 | TZS Equivalent |
| **Interest on Uncleared Effect** | **TShs** | **TShs** |
| Below 150,000 | 5,000 | 5 |
| Above 150,000 | 3% | 3% |

**Alternate Banking chanels services**

| Services | Charges |
|---|---|
| ATM mini statement | Free |
| Visa Card Application | 10,000 |
| Visa card Replacement / Reissue | 10,000 |
| Visa card Withdrawal (EBL ATM) | 1000 |
| Visa card Withdrawal (other ATM) | 3000 |
| Declined Visa card Transaction (other ATM) | nil |
| Visa card Balance Enquiry (other bank ATM) | nil |
| Cash Back Shopping | free |
| Cash Back cash withdrawal | 500 |
| Utility Bill Payments | Free |
| ATM withdrawal Limit per trx | 400,000 |
| ATM withdrawal Daily Limit | 1,000,000 |

| Mobile Banking/Eazzy 24/7 | Charges |
|---|---|
| Eazzy 247 activation | Free |
| Bill payments | Free |
| Eazzy 24 /7 Pin Change/stop a card language change | Free |
| Eazzy 24/7 Mini-statement/ Enquiries & requests | 300 |
| Eazzy 24/7 Airtime Top-up | Free |
| Eazzy 24/7 Funds Transfer(Equity to Equity account) | 2,000 |
| Eazzy 24/7 Funds Transfer(other banks) | 11,800 |
| Eazy247 funds transfers (Bank to Mobile) { TZS 1,000- TZS 100,000} | 2,000 |
| Eazy247 funds transfers (Bank to Mobile) { TZS 100,001 - TZS 200,000} | 3,000 |
| Eazy247 funds transfers (Bank to Mobile) { TZS 200,001- TZS 500,000} | 4,000 |
| Eazy247 funds transfers (Bank to Mobile) { TZS 500,001- TZS 1,000,000} | 6,000 |

| SERVICE | CURRENCY TZS |
|---|---|
| **E-banking** | **Charges** |
| E-banking balance enquiry | Free |
| Retail E-banking annual subscription | Free |
| Corporate E-banking annual subscription | 150,000 |
| Additional token key(Corporate E-banking) | 50,000 |
| E- banking Funds Transfer - retail & corporate | 2,500 |
| E-banking statement request (printed by the bank) | 1500 per leaf |
| E-banking statement request (Self downloaded) | Free |
| E-banking Pin Regeneration | Free |
| E-banking -Cheque book/bankers cheque request | Free |
| E-banking - Salary Processing | 2,000 |

**Loans & Other Credit Facilities** — Charges

| Loan Type | Interest | Interest on application |
|---|---|---|
| Salary advance (loan) | 25% | 3%-5% |
| Equiloan (chq off) | 17%-25% | 1.5%-3% |
| Farm input | 16%-23% | 2%-3% |
| Business loans | 18%-23% | 2%-3% |
| Development loan | 18%-23% | 2%-3% |
| Agricultural loan | 16%-23% | 2%-3% |
| Agricultural commercial loan | 16%-23% | 2%-3% |
| Business Overdraft | 18%-23% | 2%-3% |
| Project Loan | 18%-23% | 2% |
| Asset Finance - Retail | 13% | 2% |
| Asset Finance - Second Hand Commercial Vehicles | 13% | 2% |
| Invoice discounting | 18%-23% | 3% |
| Shares finance Loan | 18%-23% | 3% |
| Mortgage Loans Local | 18%-23% | 3% |
| Mortgage Loans-Diaspora | 18%-23% | 3% |
| School Development Loans | 18%-23% | 2%-3% |
| School Asset Finance | 13% | 2% |
| Biashara Bora/Kilimo Kisasa Loan | 16%-23% | 3% |
| Borrowing against Jijenge, FDR, (L.A.C.E)* | 5%-10%Margin | 1% |

| Fanikisha Loan Products | Interest | Interest on application |
|---|---|---|
| Fanikisha Maisha & Fanikisha Shaba | 18%-23% | 2% |
| Fanikisha Imara | 23% | 2% |
| Fanikisha Dhahabu | 18%-23% | 2% |
| Fanikisha SME | 18%-23% | 2% |
| Fanikisha Tanzanite | 18%-23% | 2% |
| **Interest on Loan Application** | | |
| 1-200,000 | 25% | 3%-5% |
| 200,001-500,000 | 25% | 1.5%-5% |
| 500,001-10,000,000 | 16%-25% | 1.5%-5% |
| 10,000,001-50,000,000 | 16%-25% | 1.5%-3% |
| >50,000,001 | 16%-23% | 1.5%-3% |
| Repeat loans | 16%-23% | 1.5%-5% |
| Corporate Loans | 18%-23% | 2% |

| Trade Finance | Charges |
|---|---|
| Bid bonds | 1% min100,000 |
| Perfomance bonds | 3% pa min 100,000 |
| Bank guarantees | 3% pa min 100,000 |
| Discharge of charge (Releasing of security) | 20,000 |
| Bid bonds extension | 50,000 |
| **Import Letters Of Credit interest** | **Charges** |
| Opening Commission | 0.75 % per quarter or part thereof min $100 |
| Swift charges | $60.00 for long message and $50 for short massage |
| Amendment | $50 |
| Extension of the LC validity | 1 % per quarter or part thereof min $100 |
| Increase in amount of credit | $50 |
| Retirement commission | 0.25% minimum $20 max $100 |
| Acceptance commission | 1 % per quarter or part thereof min $100 |
| Post import Finance Commission | 1% per quarter or part thereof plus applicable interest |
| Extension of maturity of bill - LC | 1 % per quarter or part thereof min $100 |
| Postage for LCs | $50 |
| Document Handling | $50 |
| LC discharged unutilised | $50 |
| **Export Letters Of Credit** | |
| Advising Commission | $50 |
| Confirmation commission | 1% per quarter or part thereof minimum $100 |
| LC Amendment | $50 |
| Extension Commission - Confirmed LC | 1% per quarter or part thereof minimum $100 |
| Extension Commission - Unconfirmed LC | $50 |
| Increase of Amount - Confirmed LC | 1% per quarter or part thereof minimum $100 |
| Courier charges | Tshs10000 |
| Acceptance commission - Confirmed LC | 1% per quarter or part thereof minimum $100 |
| Acceptance commission - Unconfirmed LC | 0.25% per quarter or part thereof minimum $50 |
| Retirement commission | 0.25% minimum $20 max $100 |
| Discounting of Bills | 1% per quarter or part thereof Minimum Tshs10,000. Plus applicable interest |
**The Bank was penalised Tshs 4.7 million for failure to comply with Guideline on sorting, counting, packaging cash depositing and counterfeits detection for the quarter ended 30th September 2020. We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.**

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

For more details call 080 078 0111 or visit www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
Innovation is life

# Vyuo vikuu 2 vyanufaika na mamilioni ya utafiti

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TANZANIA ni miongoni nchi yenye mabaraza saba ya maendeleo ya sayansi yaliyo kusini mwa Jangwa la Sahara, ambayo vyuo vikuu vyake viwili vitanufaika kwa kupata dola za Kimarekani milioni 2 kwa ajili kuwekeza kwenye utafiti.

Utafiti huo pia utajikita katika virusi vinavyosababisha maradhi kwa binadamu na wanyama pamoja na kupata tiba ya ugonjwa wa malaria.

Vyuo vikuu hivyo vilivyofanikiwa kuingia katika mpango huo ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilichopo mkoani Morogoro ambacho ndio kitafanya utafiti wa virusi vinavyosababisha maradhi kwa binadamu kwenda kwa wanyama wakati Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela kilichopo Arusha kitafanya utafiti ili kupata tiba ya malaria.

Akizungumza mjini hapa, kiongozi wa mradi wa kituo cha Umahili cha Utafiti wa Magonjwa Ambukizi cha nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (SACIDS-ACE), Prof. Gerald Misinzo, alisema kuwa miongoni mwa vigezo vilivyopelekea Tanzania kupata utafiti ni baada ya kushindanishwa na nchi 15 za Afrika ambazo zipo katika mpango huo, ambapo nchi saba ikiwamo Tanzania ilifanikiwa kufudhu vigezo vilivyowekwa kutokana na watafiti wake kuwa mahiri katika utafiti.

Prof. Misinzo kutoka SUA ambaye atasimamia utekelezaji wa utafiti wa virusi vinavyosababisha maradhi yanayotokana na virusi, alisema utafanyika kwa wanyama wanaoishi na binadamu ikiwamo mbuzi, kuku, samaki, nguruwe ambao wamekuwa wakifugwa na jamii kwa lengo la kuondoa magonjwa yanayoleta changamoto ili yapatiwe ufumbuzi na yasilete madhara kwa binadamu.

Alisema kupitia Mfuko wa Utafiti wa Afrika Kusini (NRF) Idara ya Sayansi na Ubunifu kwa Ushirikiano na Mfuko wa Oliver and Adelaide Tambo (OATF),Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo ya Utafiti cha Canada (IEDC) na mabaraza saba ya maendeleo ya sayansi yaliyo kusini mwa Jangwa la Sahara watafanya utafiti kwa kujenga uelewa mpana na kukuza maendeleo ya ujuzi. Naye Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema ili kuendeleza teknolojia na uvumbuzi, chuo kimeanzisha Kigoda cha Utafiti chini ya Wakfu wa utafiti wa Oliver Tambo, ambapo kupitia wakfu huo, watapata dola za Kimarekani 195,000 kila mwaka kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2020.

Prof. Chibunda, alisema hatua hiyo inatokana na mkakati wa serikali kwa kuwekeza katika utafiti na kuifanya SUA iweze kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi ili waweze kupata majawabu yatakayosaidia kuongeza tija katika maeneo mbalimbali, hivyo nchi kuondokana na umaskini.

Mratibu wa Utafiti kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Prof. Mohamed Sheik, alisema fedha hizo za utafiti zilizotolewa kwa vyuo vikuu viwili nchini zitasaidia kutumika kwa nchi za Afrika na sio Tanzania pekee, hatua ambayo itaongeza ushirikiano zaidi kwa nchi hizo.




Vyombo vya usafiri vikipita kwa shida kutokana na daraja lililopo eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam, kuharibiwa na mvua zilizonyesha hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sheikh ataka waliochaguliwa kuombewa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE Bashart Rehman Butt wa Jumuiya ya Kiislamu ya Ahmadiyya Tanzania amewaomba viongozi wa madhehebu ya dini nchini, kuwaombea wagombea wa vyama vya siasa watakaochaguliwa ili wafanye kazi ya kuleta maendeleo kwa kushirikiana.

Aidha, maombi hayo pia yatumike kuwezesha wagombea hao kuondoa tofauti zao za kiitikadi za vyama vyao vya siasa, ili kila mmoja akawajibike kwa malengo ya kuliletea taifa maendeleo.

Alisema hayo kwenye maadhimisho ya Maulid ya Mtume, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Bashart alisema maombi hayo ni muhimu kwa viongozi hao watakaochaguliwa ili kuwawezesha kuondoa tofauti walizokuwanazo kwenye mchakato wa uchaguzi mkuu. Jumuiya ya Ahmadiyya imewaomba waumini wa dini ya Kiislamu kusherehekea sikukuu ya Maulid kwa kuwakumbuka jamii ya watu wasiojiweza na wenye mazingira magumu.

Alisema moja ya mafundisho ya Mtume Mohammed ni pamoja na kuwakumbuka watu wasiojiweza, hivyo waumini wenye uwezo wanaombwa pia kuwakumbuka katika kipindi chote.

Mbali ya kusherehekea na jamii hiyo isiyojiweza, pia waumini wanatakiwa kuwakumbuka wagonjwa hosipitalini, wafungwa magerezani na watu wenye ulemavu, ambao hawajiwezi kimaisha.

Aidha, aliwataka waumini kutekeleza maadili ya kiongozi huyo kwa kuyafanya kwa vitendo ikiwamo kujiepusha na chuki na dharau kwa jamii inayowazunguka.

Alisema kuwa kuna makundi mengi hayana uwezo kwenye vipindi kama hivi vya sherehe, hivyo ni wajibu kwa waumini ambao wana uwezo kuwakumbuka ili na wao waweze kumkumbuka Mtume wao.

# TAWA kukamilisha miundombinu magofu

**Na Christina Haule,** LINDI

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imesema itahakikisha miundombinu yote ya eneo la utalii la magofu ya Kilwa-Kisiwani Songo/Mnara yanakamilika kwa wakati na kufanya kuwa na kivutio muhimu kwa wageni ili kupata watalii milioni 5 ifikapo mwaka 2025.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TAWA, Hamisi Semfuko, alisema hayo wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa miundombinu hiyo uliofanyika kwenye magofu hayo yaliyopo Kilwa-Kisiwani mkoani Lindi, ambapo alisema TAWA itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha ili kuhakikisha miundombinu yote inakamilika.

Semfuko alisema kukamilika vizuri kwa eneo hilo kutakifanya kuzidi kuwa kivutio muhimu kitakachovutia wageni zaidi na kuliingizia Taifa fedha za kigeni ili kufikia malengo yanayokusudiwa.

Alisema mwaka 2018/19 Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanya uamuzi wa kugawa mamlaka ya usimamizi wa vivutio vya malikale kwa taasisi za TAWA, TANAPA, TFS na NCAA na kuikabidhi TAWA kusimamia malikale za Kunduchi, Kilwa kisiwani na Songo/Mnara.

Alisema katika kusimamia maeneo hayo TAWA ina wajibu wa kulinda kuhifadhi na kuendeleza magofu hayo na rasilimali nyingine zilizopo kwa kuzingatia sheria za kitaifa na kimataifa kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Semfuko alisema TAWA imeandaa mpango wa utekelezaji utakaogharimu Sh. 2,132,485,000 ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye malikale hizo ikiwamo kukosekana maliwato katika hifadhi, uchakavu wa ghati la Kilwa Kisiwani na uhaba wa ghati eneo la Songa/Mnara.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, aliishauri TAWA ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ili kurekebisha miundombinu ya shule, kuweka maji na kuboresha zahanati kwa ajili ya huduma za matibabu kwa wakazi wa maeneo ya Kilwa- Kisiwani.




Ukurasa 13

Hongereni washindi, poleni washindwa

BUFE

IJUMAA OKTOBA 30, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 12

Neema ya kufufuliwa kiwanda cha kwanza kitaifa kuchakata pamba

# Watafiti wa Tengeru wanapojivunia zao ‘mchicha bhangi’ linavyong’ara

**Na Renatha Msungu,** ALIYEKUWA ARUSHA



Kilimo cha mchicha kikiendelea shambani. **PICHA: MTANDAO**

KITUO Cha Utafiti wa Mbegu za Asili za Mboga, kiitwacho World Vegetable Center Afrika Mashariki na Kusini (WORLD VEG ESA), ni miongoni mwa vituo vinavyofanya utafiti kukusanya na kuhifadhi mbegu za mboga za asili.

Ni asasi yenye makao makuu eneo la Tengeru, Arusha, kuwakilisha Afrika Mashariki na Kusini. Kimekuwa kikifanya kazi ya kutafiti na uhifadhi wa mbegu hizo na kuhamasisha watu kutumia mboga za asili kujenga afya zao.

Mkurugenzi Mkuu wa kituo hicho, Dk. Gabriel Rugalema, anaiambia Nipashe kwamba chimbuko la kituo hicho kutoka nchini Taiwan mwaka 1973, ambako kuna makao makuu ya asasi hiyo na nchini lilianzia mwaka 1992.

Dk. Rugalema anasema uanzishaji kituo hicho, ulilenga kuzuia na kudhibiti utapiamlo kwa watoto waliopo katika nchi za Afrika, ikinuia kupunguza umasikini.

“Baada kufanyika tafiti katika mboga mboga za asili iligundulika kuwa kuna virutubisho vingi na muhimu katika mwili wa binadamu, hivyo endapo mboga mboga hizo na mbegu zake zitatumiwa kwa wingi, basi tatizo la utapiamlo litaisha katika nchi za Afrika,” anasema.

Anafafanua kuwa, watafiti pia waliangalia hali ya umaskini unavyoikumba Afrika na waligundua biashara ya mboga za asili na matunda inaweza kupunguza tatizo.

“Mbogamboga na matunda ni biashara kubwa sana duniani, kwani mwili wa binadamu unahitaji virutubisho vingi kutoka kwenye vyakula hivyo,” anasema mkurugenzi huyo.

Dk, Rugabalema anasema shirika hilo linalofadhiliwa na wadau wa maendeleo kutoka nchi za Ulaya na Marekani, kwa kushirikiana na serikali limekuwa likitoa elimu kwa wakulima, jinsi ya kulima vyakula hivyo.

Mkurugenzi huyo anasema, baada ya kuona kilimo cha mboga na matunda kinashika kasi kila siku, wameshafungua tawi Unguja na wameshawafundisha kwa mafanikio, ulimaji wa vyakula hivyo.

Anataja utafiti mmojawapo uliokonga roho za wadau, ulihusu aina 82 za mchicha asili, ambazo zote zinaliwa na zina virutubisho vinavyofanana, isipokuwa katika tofauti ya ladha. Hapo ndipo kunakopatikana kinachojulikana kama ‘mchicha bhangi’ katika mashamba ya kituo hicho.

Mtafiti Msaidizi wa kituo hicho, Raphael Malogo, anasema aina ya mchicha huo majani yake yanafanana na majani ya mmea bangi, ambao ni haramu.

“Watu wengi wakisikia ‘mchicha bhangi’ wanajawa na shauku ya kujua huo mchicha una kitu gani cha ziada mpaka kuitwa hivyo? Lakini unaitwa hivyo, kutokana na mfanano wa majani yake,” anasema Malogo, anayetaja jina lingine la bidhaa hiyo kutoka Tengeru ‘Madir I’.

Anaeleza, baada ya kuufanyia utafiti ‘mchicha bangi’ sokoni, walibaini unapendwa sana na walaji kutokana na ladha yake na anasema kiuchumi, una faida nyingi kwa mkulima, anayeweza kuuchuma mara tano na unakaa muda mrefu, una virutubisho vingi kwa manufaa ya afya ya binadamu.

“Mchicha bhangi unasaidia kuondoa uono hafifu, una Vitamini C; calcium; madini ya zinki; na kuimarisha kinga za mwili,” anasema mtafiti Malogo.

Anaeleza namna ‘mchicha bangi’ unaweza kustawi katika mazingira yote, ingawa haijafahamika sana nchini akiwa na ufafanuzi: “Mchicha bhangi asili yake Zimbabwe.

Ni mboga ambayo hutumiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi wa nchi hiyo, kwa hapa chini kituo hiki ndio cha kwanza kulima.”

Hata hivyo, mtafiti huyo anataja aina nyingine ya asili, Mchicha Akheri; huo unatoa mbegu nyeupe, na faida zake ni virutubisho vingi mwilini, unaotajwa kuwa na ladha nzuri na rangi nyekundu na ulilimwa kwa ajili ya mbegu.

Madira Two; ni aina ya mchicha ambao mtafiti huyo alisema mchicha huo unalimwa kwa ajili ya mboga unavunwa baada ya siku 28 tangu kupandwa,

Mchicha Pori; huo unavunwa kila baada ya siku 21 tangu kupandwa, unachumwa mara mbili tu na baada ya hapo, kitaalamu unatajwa kutofaa. Ni mchicha uliobebeshwa jina la ‘mchicha nafaka’ ambao mbegu zake zinasagwa kuwa unga.

Mchicha Nguruma; huo unaweza kuvunwa hata mara nne katika tuta moja na una sifa ya kuchipua haraka, majani yake ni mapana mahsusi kwa mboga na inafaa kuvunwa kila baada ya wiki tatu.

Mtafiti huyo anasema, aina zote za mchicha zina virutubisho vinavyofanana, akiwashauri watu kuzitumia.

BIASHARA
KAHAMA IMEWEZA...

# Neema ya kufufuliwa kiwanda cha kwanza kitaifa kuchakata pamba

## • Mabilioni mkopo yazamishwa, yachanua • Vingine kufufuliwa...Ushirika KACU kazini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA mikoa ya Kanda ya Kati, unapozungumzia uchumi wao, basi zao pamba ambalo pia ni la kimkakati kitaifa, ndio uchumi wao wa leo.

Ndani ya Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), katika uamuzi wake kujifufua, kimetumia Sh. bilioni 3.1kati ya Sh. bilioni 4.6 ilizokopa katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), kukarabati kiwanda chake cha kuchakata pamba na kununua zao hilo kwa mkulima.

Ni hatua inayotarajiwa kufungua wigo wa ajira, matarajio ni wastani wa zaidi ya vijana 200 kuajiriwa kwa shughuli mbalimbali zinazohusiana na uzalishaji mali katika kiwanda hicho, manufaa yalianzia Kahama na kufikia maeneo ya wilaya na mikoa jirani.

Thamani ya zao la pamba itaongezwa na kuasaidia kuepuka hasara, ikiwamo zitokanazo na ushindani sokoni na uchumi wa Kahama kuanza kushika kasi.

**MWENYEKITI USHIRIKA**

Emmanuel Charahani, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), anasema chama hicho kinaundwa na vyama vya msingi (AMCOS) 59 vyenye wanachanma 12,496, walimaji wa pamba pekee na kuna vyama 42 vyenye wanachama 4,493 walima tumbaku.

Aidha, anaorodhesha vyama vingine 15 vyenye jumla ya wanachama 1,673 wanaojishughulisha na mazao yote mawili, tumbaku na pamba. Kwa kifupi KACU sasa kina jumla ya wanachama hai 18,662.

Charahani anasema, katika majumu yao wamekuwa wakiwahudumia wakulima kwa kuwatafutia masoko na kuwaunganisha na wanunuzi, kusaka pembejeo ikiwa na kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili kuwakopesha wakulima.

**UZALISHAJI/SOKO**

Mwenyekiti Charahani anasema, katika msimu wa kilimo uliopita kumekuwapo na changamoto ya kushuka uzalishaji wa zao la pamba, akitaja sababu kuu ni mabadiliko ya hali ya hewa.

Hata hivyo, anajitetea pembejeo zimekuwa zilisambazwa kwa wakati kumfikia kila mkulima na KACU inawahudumia wanachama kutoka halmashauri tatu za Kahama Mjini, Ushetu na Msalala, ambazo ni wazalishaji wa pamba na mpaka sasa kuna jumla ya kilo 700,677 yenye thamani ya Sh. milioni 629.388.

> **“ Mrajisi wa Ushirika Benson Diege, anachangia mada akisema viwanda vya ushirika vilivyotakiwa kufunguliwa vilikuwa saba na hadi anavitaja vilivyokwishafunguliwa ni KACU, Chato na MBCU.**



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na wakulima wa pamba na tumbaku, kutoka halmashauri za Msalala, Kahama Mjini na Ushetu, alipofungua kiwanda cha uchakataji pamba, Kahama.



Naibu Waziri wa Kilimo Hussein Bashe (katikati) akikata utepe kuzindua kiwanda cha uchakataji wa pamba, mali ya Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU). Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Zainabu Tellack na kulia kwake, Mwenyekiti wa Chama hicho, Emmanuel Charahani. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

Aidha, Charahani anasema, vyama vya msingi hadi sasa ndio walizalishaji kwa mchanganuo; Ushetu ni kilo 595,259; Msalala kilo 82,045; na Kahama Mjini kilo 23,374 na kufufuliwa kwa kiwanda hicho, hivi sasa kumeongeza ushindani wa masoko, pia kampuni za ununuzi wa zao hilo na kwa misimu huu.

“Kiwanda hiki kimeongoza ushindani wa masoko na kampuni ya kununua pamba katika msimu huu, kutoka kiasi cha shilingi 800 kwa kilo moja hadi Sh. 900 na kuna baadhi ya maeneo ya Kishapu na Geita, ilifika hatua tukanunua kwa kiasi cha Sh. 920 sawa na asilimia 11,” anasema Charahani.

”Lengo la kufufua kiwanda hiki ni kutatua changamoto ya ukosefu wa masoko kwa wakulima wa pamba kila msimu na kuongeza uzalishaji wa zao hilo, kutokana na kuwapo masoko ya uhakika na mkulima kuendelea kunufaika na kilimo anacholima,” anasema.

Anasema, kiwanda kilisimama uzalishaji kwa miaka saba, hata ukasababisha wimbi la ukosefu ajira katika maeneo ya Halmashauri za Kahama Mjini, Ushetu na Msalala, pia kwa walima pamba, uzalishaji ulishuka.

Charahani anaorodhesha matatizo makuu kwao, ikijumuisha upungufu wa vifungashio vya mabero ya pamba, chanzo kikuu kikitajwa ni athari za ugonjwa wa corona kimataifa, hata kukwamisha uagizaji wake kutoka nchini China.

Pia, anataja uchakavu wa mashine za kufunga robota za pamba nyuzi, unasababisha kupunguza kasi ya uzalishaji, kwani mashine hiyo imekuwa ikikarabatiwa kila mara na kuna wakati upatikanaji vipuri nao umekuwa shida.

Aidha, Charahani anasema uhaba wa pamba Kahama, ulifanya kununuliwa pamba za wilaya nyingine za Kishapu na Nyanghwale.

**RC SHINYANGA**

Zainab Telack, ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anasema kiwanda chake kimekuwa cha kwanza kitaifa kufunguliwa na kuanza kazi, hali anayotarajia kitaongeza uzalishaji wa pamba na kutatua shida ya soko.

Anasema, asilimia 80 ya wakazi wa Shinyanga, ni wakulima na kila mmoja anapaswa kunufaika na uwepo wa kiwanda, akiwasihi walimaji hao kufuata kanuni 10 za kilimo za kuhakikisha pamba safi inapatikana.

Zainab anamtaka Mwenyekiti Charahani kuhakikisha pamba ya sasa inaingia kwenye ushindani wa soko, kama ilivyo kwenye zao la tumbaku, lengo ni kumnufaisha mkulima na kilimo chake.

**BENKI NA MRAJISI**

Japhet Justin, ni Mkurugenzi wa TADB, anasema kuwa walikikopesha kiwanda Sh. bilioni 4.6 kwa riba ya asilimia 12, ili kiweze kufufua kiwanda na kununua pamba kutoka kwa mkulima.

Anasema baada ya kufunguliwa masoko ya pamba, mkakati ambao kimsingi ni sehemu ya kuyapa uhai mazao ya kimkakati, walikisimamia kiwanda hata kupandisha bei ya pamba sokoni, kufikia Sh. milioni 920 kutoka Sh. 800.

Bosi huyo wa berko anasema, pia wako katika matarajio ya kutoa mkopo mwingine wa kuanzisha kiwanda kipya cha uchakataji mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za pamba, ikitarajiwa itasaidia kuongeza uzalishaji kwa upande wa wakulima.

Mrajisi wa Ushirika Benson Diege, anachangia mada akisema viwanda vya ushirika vilivyotakiwa kufunguliwa vilikuwa saba na hadi anavitaja vilivyokwishafunguliwa ni KACU, Chato na MBCU.

Pia, anasema mwaka ujao watuenda kuvifungua viwanda vingine anavyovitaja kwa majina ya Sola, Lugula na Manawa, akiwataka wanachama wa KACU kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu yanayofanywa kiwandani, ikiwamo kudai taarifa za mapato na matumizi.

**NAIBU WAZIRI KILIMO**

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anamtaka Mkurugenzi wa Benki ya Kilimo, kufikiria kupunguza riba ya mikopo kwa vyama vya msingi kutoka asilimia 12 hadi asilimia tisa kama ilivyo kwenye zao la kahawa.

Aidha, anasema serikali imetengeneza mfuko wa pembejeo ambao fedha zake zinatokana na makato kwa kila kilo na kwamba wameanza kwenye zao la korosho ni Sh.10, tumbaku ni Sh. 200 na hivi karibu imeanzishwa kwenye pamba, fedha zikitumika kununua pembejeo.

Bashe anautaka uongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa Shinyanga (SHIRECU), kuachia mali zinazomilikiwa na vyama vya chini yake, KACU na MBCU, ili kubaki na mali itakazoweza kuzimiliki, hata kuingiza ushindani katika mazao ya kimkakati.

Rai ya Bashe, pia anavitaka vyama vikuu vya ushirika kitaifa kuhakikisha vinatafuta masoko ya zao la tumbaku katika nchi ya Zambia, kama zinavyofanya kampuni za ununuzi na kupata faidia zaidi.

“Wakulima wetu wanatumia gharama kubwa kwenye maandalizi ya kilimo, lakini mwisho wa siku wanakuja kuuza tumbaku yao kilo moja kwa dola 1.6(Sh. wastani Sh. 3500) huku wanunuzi wakienda kuuza Zambia kwa dola tano jambo ambalo mnunuzi anapata faida kubwa kuliko kulima wetu,” anasema Naibu Waziri Bashe.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hongereni washindi, poleni washindwa






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

ASALAAM aleykum Watanzania wenzangu! Tumsifu Yesu Kristu! Hatimaye Tanzania yetu imerudi kwenye reli. Tuliowataka wamekuja kilingeni kutuongoza. Bila shaka tumebaki na makovu ya hapa na pale yaliyosababishwa na uchaguzi.

Waliochaguliwa tuwapongeze na walioshindwa tuwape pole na kuwatia moyo, kwamba maisha yanaendelea na baada ya miaka mitano tukutane tena. Walioshinda wasiwabeze walioshindwa na walioshindwa wasiwanunie walioshinda.

Tunajua, pamoja na kushinda lazima kuna wasio na uwezo, ingawa kwa nguvu zake Yarabi turufu iliwaangukia na walioshindwa wapo wenye uwezo mkubwa, lakini ndivyo hivyo, walilamba garasa na kubaki kugugumia kwa maumivu, lakini siku zote nafasi inayogombewa ni moja.

Ukitaka usiumize moyo jifunze kuielewa Tanzania tu kwamba ndivyo ilivyo na utaratibu wa kuachiana na kupokezana vijiti, ingawa kwa mbilinge kubwa na nzito za kutoa machozi na damu wakati mwingine.

Wapo wanaolia kuingizwa hasara, lakini wapo wanaoangalia fursa.

Mambo yako hivyo, kwa sababu tofauti na zamani, uongozi ulikuwa ni wa kuwaambia watu ukweli na kuwasaidia kiukweli, sasa watu wanaambiwa uongo na ukweli sawia, hatimaye wasisaidiwe au kuhudumiwa, ili mradi mtu keshaingia, kutoka ni miaka mitano. Yailahi!

Mambo ya leo ni mtu kuangalia kwanza tumbo lake, ndipo akisaza amwangalie na mwingine aliye jirani kabla ya kumfikia aliye mbali. Ndiyo maana wachaguliwa wakishakalia vilivyo vyao, husahau waliowakalisha hapo na kuangalia mambo yao ya Tumbo Street!

La kufanya kwa wachaguaji au wapiga kura, ni kurudi kwenye ahadi na ilani na kuangalia kimoja baada ya kingine na kukifuatilia kwa mintarafu ya kauli za wagombea na kudai haki hata kwa kupiga kelele, kwa sababu ndiyo njia pekee kabla ya miaka mitano mingine kutimu.

Ieleweke, kwamba baada ya uchaguzi katika nchi yoyote mbali na kutibu majeraha, ndipo wachaguliwa hufunua makucha na kuonesha makaliyao, lakini rangi zao halisi na kufanya wanavyohisi na si wanavyotaka mabosi waliowachagua.

Ndio wakati ule wahenga walisema majuto ni mjukuu, kama ulichagua sura ndipo sasa utaona jinsi sura hiyo itakavyokutazama na iwe nafuu kama utaiona mtaani kwako na kama ulichagua pesa, ndipo utaona kama pesa hizo zitafika kukusaidia kutatua shida na kero ulizonazo.

Lakini ni vyema, kwamba wakati baada ya uchaguzi ndio pia wakati wa kujifunza kutokana na makosa, ili baadaye ujue kuwa ni ujinga pa kwenda lakini werevu pa kurudi. Sawa na kusema kutenda kosa si kosa, bali kurudia kosa.

Ingawa kipindi cha uchaguzi watu hubadilika na kuwa na kauli laini zenye ahadi tamu, hubadilika sura na kuwa wanyenyekevu na wanyonge mbele ya wapiga kura na kuomba kuchaguliwa kwa kupiga magoti na kusujudu, lakini ni vyema kuwa makini ili kosa lisijirudie.

Ni jukumu la aliyepewa ufunguo wa Ikulu sasa, kujipanga kuona kuwa anakuwa na wasaidizi watakaofanya anachokitaka kwa maslahi mapana ya wanaoongozwa, ili asijesababisha majuto kwa wapiga kura kulilia kura walizopoteza kwa ajili yake.

Pia, ni matumiani ya walio wengi, kwamba waliopewa dhamana hizo hawatazikalia na kuzitumia kujikomba kwa walio karibu nao, kama ndugu, jamaa na marafiki na waliowapigia kampeni, badala ya kusaidia Watanzania wote.

Na wala wasijetumia fursa hizo kukandamiza walio na itikadi tofauti, kwa kuamini tu kwamba hawakuwapa kura, kwa sababu tunajua wengi wape lakini wachache nao wasikilizwe. Kila mtu astahili keki ya Taifa lake analolitolea jasho kila kukicha.

Kuna usemi maarufu unaotumiwa na wanasiasa ingawa naamini huwa hawauzingatii kiroho, kwamba tunajenga nyumba moja tusigombanie fito. Ni kauli mwanana iliyojaa dhana ya mshikamano na umoja, lakini inahitaji dhamira ya dhati kuitekeleza.

Viongozi wenye hila na roho mbaya, ndio hao wasioweza kuizingatia kauli hiyo na mara tu waingiapo madarakani, huamua kung’ang’ania fito, na kutaka kujijengea kijumba na kuacha nyumba ikiporomoka. Hatutarajii hilo litokee katika nji hii ya Kambarage. Alamsiki!

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2020

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.06.2020 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,984 | 4,728 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,531 | 18,343 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 20,859 | 20,883 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 40,769 | 35,257 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 5 | 16 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 124,342 | 102,357 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,448 | 4,275 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,202 | 1,250 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **209,140** | **187,109** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 24,248 | 11,504 |
| 18 | Amana za Wateja | 139,947 | 127,814 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 77 | 79 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 32 | 40 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 39 | 39 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,385 | 5,661 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **166,728** | **145,137** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **42,412** | **41,972** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 28,654 | 28,733 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,935 | 2,242 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 823 | 997 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,412** | **41,972** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 9,423 | 8,388 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,590 | 2,585 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,637 | 1,366 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20% | 22% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2% | 2% |
| (iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77% | 74% |
| (iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 59% | 55% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89% | 85% |
| (vi | Ongezeko la Amana | 18% | 3% |
| (vi | Ongezeko la Mali | 12% | 5% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2020

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | ROBO YA MWAKA SASA 30.09.2020 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 30.09.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2020 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.09.2019 |
|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 3,748 | 3,749 | 11,203 | 10,798 |
| Gharama za Riba | 1,356 | 1,267 | 3,922 | 3,550 |
| **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,392** | **2,481** | **7,281** | **7,248** |
| Madeni Viza yaliyofutwa | - | - | 34 | - |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 271 | 330 | 743 | 1,110 |
| **Mapato yasiyo ya Riba:** | **277** | **180** | **1,032** | **1,335** |
| 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na | | | | |
| Miamala ya Fedha za Kigeni | 110 | 149 | 318 | 476 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 163 | 27 | 704 | 850 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 4 | 4 | 10 | 8 |
| **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,339** | **1,405** | **3,668** | **4,021** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 533 | 600 | 1,617 | 1,771 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 177 | 13 | 257 | 263 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 629 | 793 | 1,794 | 1,987 |
| 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,060** | **926** | **3,869** | **3,452** |
| Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 366 | 933 | 1,098 |
| **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **694** | **560** | **2,935** | **2,354** |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **694** | **560** | **2,935** | **2,354** |
| Idadi ya Waajiriwa | **50** | **48** | **50** | **48** |
| Mapato kwa Hisa | 69 | 56 | 294 | 235 |
| **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | 2% | 2% | 2% |
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7% | 10% | 9% | 9% |
| Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 50% | 46% | 44% | 44% |
| Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5% | 6% | 6% | 6% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 30.09.2020

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **30.09.2020** | **30.06.2020** | **30.09.2020** | **30.09.2019** |
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,060 | 1,587 | 3,869 | 3,452 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 332 | 232 | 894 | 1,254 |
| | -Prior Period Adjustment | (253) | 326 | 73 | (70) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (22,255) | (150) | (11,433) | (6,879) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | (4) | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 12,133 | (3,787) | (9,744) | 8,425 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 9,458 | 11,539 | 18,779 | 5,464 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (5,674) | 1,596 | (4,719) | (4,300) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (366) | (366) | (933) | (1,098) |
| | -*Mengineyo (Bainisha)* | (1,162) | (911) | (1,162) | (912) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(6,728)** | **10,066** | **(4,379)** | **5,335** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (13) | (9) | (31) | (26) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 24 | 3,223 | 312 | (5,801) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | -*Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **11** | **3,214** | **282** | **(5,827)** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | -*Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(6,716)** | **13,280** | **(4,098)** | **(492)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 48,517 | 35,237 | 45,898 | 31,307 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **41,801** | **48,517** | **41,801** | **30,815** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **249** | **39,404** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,935 | - | - | - | 2,935 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 200 | (200) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 73 | - | - | - | 73 |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **31,589** | **575** | **-** | **249** | **42,412** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 24,134 | 3,984 | 937 | - | 39,055 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,103 | - | - | - | 1,103 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 3,209 | (3,209) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Ziada ya Uthaminishaji wa mali zisizohamishika | | | | | | 249 | 249 |
| Mengineyo | - | - | (1,002) | - | - | - | (1,002) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **249** | **39,404** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2020**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 9th October, 2020 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 9th October, 2020 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 9th October, 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 9th October, 2020 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 9th October, 2020 |



# Korea kuyajengea uwezo makundi maalum

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI ya Jamuhuri ya watu wa Korea Kusini imepanga kuvijengea uwezo na kuvitafutia fursa mbalimbali za ndani na nje ya nchi vikundi vya vijana, walemavu pamoja na wanawake 1,000 mkoani Dodoma.

Katibu mkuu wa vikundi hivyo, Christopher Dioniz, aliyasema hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Dioniz alisema vikundi hivyo 1,000 vitaunganisha katika kikundi kimoja cha kijiji kipya cha maendeleo ambacho tayari kimeshasajiliwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Vikundi hivi vitakuwa chini ya jina hilo la kijiji kipya cha maendeleo na hili jina linatoka na neno la Kikorea la (Seamaul Undong) na hiki ni kikundi ambacho kipo pia kule Korea Kusini ambacho kimenufaisha sana watu wa jamii za chini kama sisi hapa," alibainisha Dioniz. Alisema kupitia umoja wa vikundi hivyo, wataweza kuunganisha nguvu zao kwa pamoja katika kuboresha shughuli mbalimbali za kiuchumi za kiujasiriamali, kuweka mifumo ya uratibu, ufuatiliaji na tathimini. Pia, alisema kikundi hicho kitakuwa kiungo na mwakilishi kati ya vikundi vilivyounganishwa na kampuni, taasisi za umma na sekta binafsi nje na ndani ya nchi.

"Uzinduzi wa kikundi hiki tunapanga kuufanya Januari, mwaka ujao na hii ni kutokana na nchi yetu hivi sasa kuwa katika mchakato wa uchaguzi mkuu kuwapata viongozi wapya watakao liongoza taifa hili tena kwa kipindi cha miaka mitano," alisema Dioniz.

Aidha, alisema wameamua kufanya uzinduzi huo mapema mwakani, ili kutoka fursa kwa viongozi mbalimbali wakuu wa nchi kushiriki katika tukio hilo. "Katika uzinduzi huu pia atakuwapo balozi wa Korea Kusini nchini, hivyo tunataka viongozi wetu wakuu wa nchi wasiwe na jukumu jingine kama tulilonalo hivi sasa, ili uzinduzi ufanyike kwa mafanikio makubwa na wageni wetu wasipate changamoto yoyote," alieleza.

Katibu mkuu huyo, alisema wamepata fursa hiyo kutoka serikali ya Korea Kusini kutoka na vikundi vingi jijini Dodoma, kufanya vizuri katika mikopo ya asilimia kumi, ambayo imekuwa ikitolewa bila riba na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Mpaka hivi sasa kwa kipindi cha miaka mitano Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imetoa kiasi cha Sh. bilioni 5.2 kwa ajili ya vikundi vya vijana, wanawake pamoja na walemavu, ambazo zimewawezesha kujikwamua kiuchumi," alisema.

# Mkandarasi apewa tarehe kuukabidhi mradi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imemwagiza mkandarasi wa kampuni ya Mohammedi Builders anayejenga mradi wa jengo la kitega uchumi 'Government City Complex' utakaogharimu Sh. bilioni 18, kwa awamu ya kwanza kuukabidhi ifikapo Desemba 30, mwaka huu.

Agizo hilo limetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alipoongoza timu yake ya menejimenti kutembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa kitega uchumi wa jiji 'Government City Complex' kilichopo mji wa serikali eneo la Mtumba.

"Nimekuja na timu ya menejimenti ninayoiongoza hapa kumsimamia na kumkumbusha mkandarasi anayejenga mradi huu, kuwa kwa mujibu wa mkataba wetu, mradi huu unatakiwa kuisha tarehe 30, Desemba, 2020 na bahati nzuri yeye anasema hana tatizo na kukamilisha mradi huu tarehe hiyo," alieleza Mafuru.

Pia Mafuru alisema kuwa mradi huu umejengwa katika mji wa serikali uliopo makao makuu eneo la Mtumba ili kuwezesha kutoa huduma katika eneo hilo.

"Lengo la mradi huu ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati yeye anapambana kujenga ofisi za serikali hapa Mtumba, sisi Jiji tunapambana kuhakikisha huduma ambazo zitakosekana kwenye maeneo mengine zinapatikana katika jengo hili.

"Jengo hili lina awamu nne, hii ni awamu ya kwanza ambayo tumekuja kuishuhudia ikiwa inaelekea ukingoni, nimetaarifiwa kuwa awamu hii ujenzi wake umefikia asilimia 60," alisema Mafuru.


# BANK OF BARODA (TANZANIA) LIMITED

BANKING WITH PASSION

## DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS(DISCLOSURES) REGULATIONS 2014
## CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM

**To , The Esteemed Customers Bank of Baroda (Tanzania) Ltd Tanzania**

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**
The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve com-plaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is in-tended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK(JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**
When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

| | |
|---|---|
| The Chief Manager<br>Dar es Salaam Branch<br>Post Box 5356 Dar es Salaam<br>Phone : +255 (22) 2124461; Fax: +255 (22)2124456<br>E Mail : bobdar@bankofbaroda.com | The Sr. Branch Manager<br>Arusha Branch<br>Plot No.12 Block-E, Goliondoni Road<br>Post Box 3152 Arusha Tanzania<br>Phone : +255 (27) 2544986; Fax: +255 (27)2544955<br>E Mail :bobaru@bankofbaroda.com |
| The Branch Manager<br>Kariakoo Branch<br>Crossing of Msimbazi and Mafia Street<br>Plot No.08 Block-13,<br>Post Box 5610 Dar es Salaam, Tanzania<br>Phone : +255 (22) 2185721;+255 (22) 2125390 Fax: +255 (22) 2185403<br>E Mail :bobkar@bankofbaroda.com | The Branch Manager<br>Mwanza Branch<br>Plot No.153 Block-T,<br>Kenyatta Road<br>Post Box 1914 Mwanza<br>Phone : +255 (28) 2501421;<br>+255 (28) 2501423Fax: +255 (28)2501422<br>E Mail :bobmwa@bankofbaroda.com |
| The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell, Bank of Baroda (Tanzania) Ltd<br>Post Box 5356 Dar es Salaam, Phone : +255 (22) 2124456;<br>Fax: +255 (22)2124457, E Mail :Risk.tanzania@bankofbaroda.com | |

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No. 1
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**
We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT)(NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**
If you are dissatisfied with the decision of our bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:

a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.
b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246
Note:
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**
The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**
Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**
In terms of the Guidelines issued , the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT(TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**
a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT ( KUFUTA LALAMIKO)**
A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdrawal his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**
Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**
The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**
The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

**When Aggrieved by Desk decision**
Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk.

*********************************

## DISCLOSURE UNDER REGULATION 11 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES/FEES/PRODUCTS AND SERVICES

| DESCRIPTION | | Revised Charges | |
|---|---|---|---|
| Remittances (Outward) | | TSHS | USD/GBP/EUR |
| Outward Remittances (Rapid Fund to India) | | BOB to BOB | BOB to Other Bank |
| Upto USD 5000 | | 12.00 | 18 |
| USD 5001 to 10000 | | 24.00 | 30.00 |
| Above USD 10000 | | 0.24% maximum USD 180 | @ 0.30% maximum USD 200 |
| REVISED CHARGES ( TANZANIA) | | | |
| | | In TZS | IN USD |
| Remittances (Outward) TT | INDIVIDUAL | | Upto USD or equivalent upto USD2000 -USD 13.20 USD5000 -USD 20.00 USD10000 -USD 33.00 Above USD 10000-USD 65 Flat + USD 35 Swift Charges |
| | CORPORATE | | Upto USD or equivalent 10000-USD 20.00 50000-USD 33.00 >50000-65 USD + USD 35 Swift Charges |
| Remittances (Inward) TT for Acctt Holders only | | | |
| | From Tanzania | No Charges | No Charges |
| | Outside Tanzania | | |
| | Current Acctt. / Overdraft | N.A. | 0.30% Min 12 and Max. USD 70 |
| | Saving Bank Acctt. | N.A. | Flat USD 18 |
| FBC-C | Current Acctt. /Overdraft | N.A | 0.30 % min 12 and Max. USD 70 + Postage USD 90 |
| | Saving Bank Acctt. | N.A | Flat USD 18 + Postage USD 90 |
| FBP-C | Current Acctt. /Overdraft | N.A | 0.30 % Min 12 and Max USD 70 + Postage USD 90 |
| | Saving Bank Acctt. | N.A. | Flat USD 18 + Postage USD 90 |
| TISS (Only for Acctt. Holders) Outward remittances | | 11800 | Equivalent to TZS.10000+VAT |
| Issue of Bankers Cheque Bankers payment | | 30000 | 24.00 |
| Cancellation of Bankers Cheques | | 20000 | 15.00 |
| Stop payment of Cheque | Current/OD Account | 30000 | 24.00 |
| | Saving Acctt | 18000 | 15.00 |
| Financial Reason | | 30000 | 30.00 |
| Non-Financial | | 18000 | 18.00 |
| Special clearance (DSM only) | | | |
| With in City Centre | | 72000 | 42.00 |
| Outside City Centre | | 90000 | 60.00 |
| Inward Cheque charges in clearing per Instrument | | 150 | Equivalent to Tsh.150 |
| Outgoing EFT charges | | 100 | Equivalent to Tsh.100 |
| Balance confirmation Letter | Current/OD Acctt | 18000 | 18.00 |
| | Saving Acctt | 12000 | 12.00 |
| Reference/Identity Letter | | | |
| Current/OD Acctt | | 25000 | 25.00 |
| Saving Bank | | 12000 | 12.00 |
| Cost of cheque per leaf | Current/ OD Acctt | 830 | 0.55 |
| | Saving Bank | | |
| Ledger Folio Charges | | | |
| Current / Overdraft Account | | 6000 per folio Min 6000 p.m. | USD 4 per folio Min USD 4 p.m.. |
| Ledger Charges for Savings Bank a/c | | 9000 H /Yearly | 9.00 H/Yearly. |
| For purpose of Current Account/overdraft 30 entries will constitute one ledger folio. | | | |
| Minimum Balance Charges | | | |
| Charges for not maintaining minimum balance in Current account | | 18000 p.m. | 15.00 p.m. |
| Charges for not maintaining minimum balance in Savings Bank account. | | 7500 p.m. | 7.50 p.m. |
| Acctt. maintenance charges for Saving and Current account. | Current Acctt | 18000 H/Yearly | 18.00 H/Yearly |
| | Saving Acctt | 9000 H/Yearly | 9.00 H/Yearly |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Acctt Statement | | Once in a month no Charge (Regular) | |
| Interim Acctt statement | | 6500 | 6.50 |
| Account Closure within 12 Months | Saving Bank | 25,000 | 25.00 |
| | Current Account | 60,000 | 60.00 |
| Account Closing Saving | | 18,000 | 18.00 |
| Account Closing Current | | 42,000 | 42.00 |
| Dormant Acctt Charges | Saving Bank | 3000.00 H. Yearly | 2.50 H. Yearly |
| | Current Account | 6000.00 H. Yearly | 5.00 H. Yearly |
| Upcountry Collection of cheques | | 0.6% of value (Min Commission 18000 + Postage Tzs 90000 | 0.6% of value ( Min Commission USD 18 + Postage USD 90 |
| Cash Deposit Charges | Current Acctt. | Upto 25 Mn free,60,000 upto 50 Mn 120,000 upto 100 Mn,180,000 upto 150 Mn ,240,000 upto 200 Mn ,280000 upto 250 Mn above 250 Mn 600000. | 0.30% above USD 10000 per day. |
| | Saving Acctt. | | 0. 18% above USD 5000 per day |
| Cash withdrawal Charges | Current Acctt. | Upto 25.00 Mn no charges above 25.00 Mn 0.12% of withdrawal. | 0.60 % upto 10000 and 1.18% above 10000 USD |
| | Saving Acctt. | | Upto USD 2000 no charges upto 5000 @ 0.30% and above 5000 @ 0.60%. |
| DVANCES | | | |
| ADVANCES PROCESSING CHARGES | | | |
| TZS | FCY | | |
| UPTO 10 Mn | UPTO USD 10000 | 20000 | 20.00 |
| 10 Mn to 200 Mn | USD 10000 to USD 200000 | 2.65% | 2.65% |
| Above 200 Mn | Above USD 200000 | 1.50% (Minimum 5.30 Mn) | 1.50 (Minimum 5300) |
| Loan/Overdraft against deposit of our Bank (Ist / IIIrd Party) - Waiver of Processing and documentation charges. | | | |
| DOCUMENTATION CHGS | | | |
| UPTO 10 Mn | UPTO USD 10000 | 30000 | 18 |
| 10 Mn to 200 Mn | USD 10000 to USD 200000 | 0.30% (Minimum 0.60 Mn) | 0.30% Min 30 |
| Above 200 Mn | Above USD 200000 | 0.18% (Minimum 1.18 Mn) | 0.18 % Min 600 |
| Reshedulement Charges | | 1.20% Max 1.00 Mn | 1.20% Max USD 600.00 |
| Inspection Charges | Upto Tzs 200 Mn or USD 0.20 Mn | 35000 | USD 35 |
| | Above Tzs 200 Mn or USD 0.20 Mn | 65000 | USD 65 |
| | | In addition to above inspection charges out of pocket expenses are also to be charged. | |
| Balance/Interest Certificate | | 18,000 | 18.00 |
| Prepayment Charges Principle Outstanding for residual Period) | Upto 200 Mn or USD 200000 | 2.40% p.a. | 2.40% p.a. |
| | Above Tzs 200 Mn or USD 200000 | 1.20% Subject to Min. 120000 | 1.20% Subject to Min. USD 120 |
| Bankers opinion /Confidential Report | | 30000 | 30 |
| Registration of Loan Agreement with Bank of Tanzania | | N.A. | UPTO 1 Mn USD-120 USD 1 Mn to 2 Mn- 300 USD Above 2 Mn -600 USD |
| Commitment Charges | | 1.32 of undrawn portion in case 50% average limit not utilized per quarter. | 0.66 of undrawn portion in case 50% average limit not utilized per quarter. |
| Modification Charges | | 0.12% Sanctioned Limit. Minimum 120000 | 0.12% sanctioned limit Minimum USD 60. |
| Interchangeability | | Upto 100 Mn -60000 p.a. Above 100 Mn 120000 p.a. | Up to USD 500000 USD 60 p.a. Above USD 500000 USD 120 p.a. |
| BANK GUARANTEE | | | |
| Financial/Performance per Quarter-Part of quarter treated as full quarter. | Financial | 1.35% Minimum per quarter or part thereof Min Tzs 18000 | 1.35% minimum per quarter or part thereof Min USD 15 |
| | Performance | | |
| Extension of BG | | Above commission for change in period /amt. | Above commission for change in period/amt |
| | | 1.35% of BG amt for residual period of guarantee subject to min 18000 in case of any other parameter amended. | 1.35% of BG amt for residual period of guarantee subject to min USD 15 in case of any other parameter amended. |
| BG against 100 Cash Margin | | 50% of above charges | 50% of above charges |
| Bank Guarantee | | Swift charges USD 42 or equivalent applicable in addition to above charges. | |
| Bank Guarantee Confirmation | | 75% applicable charges + USD 42 Swift Charges | |
| Documentary Credit | | IN FCY ONLY | |
| Issuance of L/Credit | | 1.35% per quarter or part there of. This period includes the usance period in case of Usance LC's+ USD 42 or equivalent swift charges. | |
| LC against 100 Cash Margin | | 40% of above charges | |
| LC Amendment | | For period and amount the above commission + USD 42 or equivalent swift charges. | |
| | | 0.42% of LC amt Min 60 USD and Maximum USD 360 or equivalent commission per amendment + USD 42 or equivalent swift charges.( | |
| | | Applicable for 100% cash margin also) | |
| Advising LC | | USD 130 and or equivalent + USD 42 or equivalent swift charges. | |
| LC Confirmation | | 1.00% per quarter or part there of This period includes the Usance period in case of Usance LC's + USD 42 or equivalent swift charges. | |
| IMPORTS/EXPORTS Bill | | | |
| Inward Bill (Under-LC) | | 0.35% + Swift Charges 42 subject to Minimum charges USD 120 | |
| | | USD 65 in addition to above charges for Discrepancy. | |
| Inward Bill (Non-LC) | | 0.65% + USD 20.00 Handling Charges + 35 Swift Charges. | |
| | | USD 65 in addition to above charges for Discrepancy. | |
| Exports Bill (Under-LC) | | 0.35%+ 42 Swift Charges+ USD 65courier Charges –Minimum USD 120. | |
| | | USD 60 in addition to above charges for Discrepancy. | |
| Exports Bill (NON-LC) | | 0.65% + 42 Swift Charges + USD 65 courier Charges subject to Minimum USD 120. | |
| | | USD 65 in addition to above charges for Discrepancy | |

| Security charges (T Bill and T Bonds) | | | |
|---|---|---|---|
| | Bidding | NIL | TZS.35000 |
| | Transfer | NIL | TZS.65000 |
| | Lien Creation | NIL | TZS.65000 |
| | Lien Release | NIL | TZS.65000 |
| SALARY PROCESSING | | TZS 1200 | USD 1.20 |
| Change of Operational Instruction | C. ACCTT | TZS 30000 | USD 30.00 |
| | SB.ACCTT | TZS 12000 | USD 12.00 |
| S.I. Failure CHGS | C.ACCTT | TZS 6000 | USD 2.40 |
| | SB.ACCTT | TZS 1800 | USD 1.20 |

**INTEREST RATES ON DEPOSITS**

| Saving Bank Deposit | Baroda Premium Current account | Weka hata Kiasi Kidogo Kinachopatikana | Short & Fixed Deposit |
|---|---|---|---|
| 2.5% p.a. for Tshs<br>0.25% p.a. Usd | -2% p.a. for maintaining min bal of Tshs 100Mn above Tshs 25mn<br>-0.25% p.a. for maintaining minimum balance of Usd 100,000 above Usd 20,000 | Rate of interest is equivalent to FDR rates for the relevant periods | Period / % per annum<br>-7 to 30 days 3%<br>-31 to 90 days 4%<br>-91 to 180 days 5%<br>-181 to less than year 6%<br>-1 year to less than 3 years 7%<br>-2 years to less than 3 year 8%<br>-3 years and above 9% |

For deposits to Foreign Currency

| Period (days) | Usd | Gbp | Eur |
|---|---|---|---|
| | (1% per annum) | | |
| 31-180 | 1.00 | 1.00 | 0.50 |
| 181-360 | 1.50 | 1.50 | 1.00 |
| 361-720 | 2.00 | 2.00 | 1.50 |
| 721 & above | 1.00 | 1.00 | 1.50 |

(I) HIGHER DEPOSITS ABOVE 50MILLION ARE WELCOME AT MUTUALLY NEGOTIABLE RATE OF INTEREST

(II) 0.50% ADDITIONAL RATE OF INTEREST ON CHARITABLE AND COMMUNITY DEPOSITS.

**INTT RATE ON LOANS ADVANCES.**

| TANZANIAN SHILLING | UNITED STATES DOLLERS |
|---|---|
| PRIME LENDING RATE – 13% MAX SPREAD-6% | 4.5% OVER 3 MONTHS LIBOR MAXIMUM 12% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**PRODUCTS AND SERVICES**

| Deposit Products | | Loan Products (Fund Based) |
|---|---|---|
| Current Deposits Account | For Banks | Finance for Corporate |
| | For Ordinary – Others | Loan for Small and Medium Enterprises |
| | Premium Account | Home Loan (Purchase and Renovation) |
| Savings Deposit | Ordinary/Others Account | Loan for Professionals |
| | Baroda Shule Account | Personal loan to Individual Salaried Employees |
| | No Frills Account | Loan to Retail Traders |
| Time Deposits | Short Deposits Scheme | Loan for Self-Employed persons |
| | Fixed Deposits Scheme | Education Loans for Specialized Courses and University Students |
| | Weka Hata Kiasi Kidogo Kinachopatikana Deposit Scheme | Education Loans for student going abroad |
| Treasury Function | | Advance Against Property |
| Money Market Producing such as Deposits and Investment in Government Securities. Dealing in Currencies (Foreign Exchanges). Import and Exports Bills. | | Loan against shares listed in stock exchange for individuals/Joint Borrowers. |
| REMMITTANCES (Fund Transfer) | | Loans for companies against shares listed in stock exchange. |
| Banker Cheque, Electronic Fund Transfer, Swift Transfer, Rapid Fund to India, Tanzania Inter-Bank Settlement System. | | Personal / Car loan to staff |
| | | Loan against future Rent Receivables |
| | | Loan against Bank's own Deposit |
| | | Insurance Premium Financing |
| | | Loan Products (Non - Fund Based) |
| | | Issuance of Letter of Credit and Bank Guarantee |

| MOBILE BANKING CHARGES | |
|---|---|
| Utility payments | |
| 1 Prepaid Airtime, SMILE 4g | 8% |
| 2 THORNLUX, TIGO prepaid airtime | 6% |
| 3 ZUKU, ZMUX | 2% |
| 4 TTCL prepaid data/voice recharge | 10% |
| 5 STARTIMES, IBE Services | 4% |
| 6 e-Water, DSTV | 3% |

| | Tariff per Transaction (VAT Inclussive) | |
|---|---|---|
| 1 | Bank2Wallet | TZS 1200 |
| 2 | Travel payments | TZS 1200 |
| 3 | NHC,UTT,PPF payments | TZS 1200 |
| 4 | Domestic Tax Payments | TZS 1200 |
| | Cardless ATM (VAT Inclussive) | |
| | TZS 5,000 to TZS 400,000 | TZS 1300 |

| Name | Designation | Date |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir | MANAGING DIRECTOR | 9th October, 2020 |
| Deogratias Edward Ndushi | HEAD OF FINANCE | 9th October, 2020 |





## Wafuasi CCM, CHADEMA wajeruhiwa kwenye vurugu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema licha ya uchaguzi kufanyika kwa amani na utulivu, kuna baadhi ya matukio ya wafuasi wa vyama vya siasa kushambuliana hasa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema matukio hayo yalitokea katika baadhi ya maeneo ya majimbo ya Kyela na Mbeya Mjini hasa siku moja kabla ya uchaguzi kufanyika.

Alisema katika Wilaya ya Kyela, wafuasi wa CCM na CHADEMA walishambuliana kwenye kata za Ipinda na Makwale ambako baadhi ya wafuasi wa CHADEMA walijeruhiwa na kulazwa hospitalini kutokana na majeraha waliyoyapata.

"Hawa walikutana kwenye zile wanaita kampeni za nyumba kwa nyumba na kwenye kushambuliana huko, wafuasi watano wa CCM waliumizwa na wa CHADEMA sita na baadhi yao wamelazwa hospitalini," alisema Kamanda Matei.

Alisema jeshi hilo linaendelea na msako, ili kuhakikisha wote waliohusika kwenye vurugu hizo wanatiwa nguvuni kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Katika Jiji la Mbeya, Kamanda Matei alisema vurugu zilitokea katika Kata ya Itezi wakati wafuasi wa CHADEMA wanatoka kufunga kampeni, walipita kwenye ofisi za CCM na kufanya fujo zilizosababisha kuanza kushambuliana na vijana waliokuwamo kwenye ofisi hizo.

Alisema vurugu hizo zilihamasishwa na kijana mmoja ambaye alimtaja kwa jina la Bon mkazi wa Uyole na kwamba jeshi hilo linaendelea kumsaka ili achukuliwe hatua za kisheria.

Matei alisema chanzo cha vurugu hizo ni vyama hivyo vyote kujiandalia walinzi ambao wanaanza kufanya kazi ambazo zilipaswa kufanywa na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola.

Vilevile bila kumtaja jina, eneo analoishi wala jimbo, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja ambaye alikamatwa kwenye kituo kimojawapo cha kupigia kura akiwa na silaha.

Alisema mtu huyo haijulikani alibeba silaha hiyo kwa sababu gani na hivyo akawataka wananchi kuepuka kufanya vitendo hivyo, huku akisisitiza kuwa Jeshi la Polisi ndilo pekee linaruhusiwa kuwa na silaha kwenye vituo vya kupigia kura.

# Tulia atangaza kuwasamehe waliomtukana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE mteule wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tulia Akson, ametangaza kuwasamehe wagombea wa vyama vya upinzani na wafuasi wao waliokuwa wanamtukana wakati wa kampeni.

Aliyasema hayo jana asubuhi alipokuwa anazungumza na vyombo vya habari baada ya kutangazwa kuwa mshindi wa nafasi hiyo kwa kuwagaragaza wapinzani wake wanne akiwamo Joseph Mbilinyi 'Sugu', aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 10.

Dk. Tulia alisema wakati wa kampeni baadhi ya wafuasi wa vyama vya upinzani walikuwa wanamtukana kiasi kwamba akiwa binadamu, alikuwa anakasirika na kutamani kuwachukulia hatua, lakini akawa anavumilia.

Alisema kwa sasa amewasamehe na atakuwa tayari kushirikiana na yeyote kuwaletea wananchi wa jimbo hilo maendeleo ikiwa ni pamoja na kumshauri namna bora ya kushughulikia kero za wananchi.

"Yawezekana walikuwa wanannitukana kwa sababu mimi ni mwanamke. Kwa kweli nilikuwa nafikia hatua nachukia sana na kutamani kujibu mapigo. Kwa sasa naomba niwaambie tu kwa dhati ya moyo wangu natangaza kuwasamehe," alisema Dk. Tulia.

Aliwataka waliokuwa wagombea wa jimbo hilo kupitia vyama vya upinzani kushirikiana naye katika kuwaletea wananchi wa Mbeya kwa kumpelekea vitu ambavyo wanatamani kuboreshwa wananchi watakuwa wametatuliwa kero zao.

Baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzania, walimpongeza Dk. Tulia kwa ushindi huo wakidai kuwa uchaguzi huo ulifanyika kwa huru na haki.

Mmoja wa wagombea hao, Protas Mgimbila, kutoka katika Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), alisema hana wasiwasi wowote juu ya mchakato wa uchaguzi na hivyo anaamini kuwa Dk. Tulia alishinda kwa haki.

Alisema kwa sasa kinachotakiwa ni kuhakikisha anatekeleza ahadi zake ili wananchi wanufaike na kura walizompigia huku akiwataka wagombea wenzake kushirikiana naye.

"Binafsi nimeridhika na mwenendo wa uchaguzi, kinachotakiwa kwa sasa tutamuunga mkono dada yetu kwa kipindi hiki cha miaka mitano, ili asipate kikwazo kwenye kuwaletea wananchi maendeleo," alisema Mgimbila.

Hata hivyo mpinzani mkubwa wa Dk. Tulia, Sugu, ndiye mgombea pekee hakuwapo kwenye ukumbi wa kujumlishia kura na wala hakupatikana kwa ajili ya kuzungumzia suala hilo.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo, Amede Ng'wanidako, alisema idadi ya wananchi waliokuwa wamejiandikisha kupiga kura walikuwa 292,580, lakini waliojitokeza kupiga kura walikuwa 114,979 na kura 1,633 ziliharibika.

Alisema Dk. Tulia alishinda kwa kupata kura 75,225 akifuatiwa na Sugu ambaye alipata kura 37,591, Mgimbila wa CHAUMA kura 236, Imani Kaili wa NCCR-Mageuzi kura 206 na mgombea wa Chama cha Wananchi (CUF) Japhet Ngode alipata kura 88.

Dk. Tulia anakuwa mbunge wa kwanza mwanamke kuongoza jimbo hilo, tangu lilipoanzishwa ambapo kabla ya Sugu lilikuwa linaongozwa na Benson Mpesya (CCM) ambaye aliongoza kwa miaka 10.



Mbunge mteule wa Jimbo la Mbeya (CCM), Dk. Tulia Ackson (kulia), akisaini karatasi ya matokeo baada ya kutangazwa mshindi kwa kupata kura 75,225 na kuwapita wapinzani wake, akiwamo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, kwa tiketi ya CHADEMA, Joseph Mbilinyi 37,591. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TARI yajipanga kusambaza mbegu bora

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole Mbeya, imeanza maandalizi ya kusambaza teknolojia za kilimo na mbegu bora za mazao mbalimbali kwa wakulima katika msimu mpya wa kilimo wa 2020/21.

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo jana, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi hayo. Alisema wameandaa mbegu za kutosha kwa ajili ya kuzisambaza kwa wananchi.

Alisema wameandaa mbegu za maharage katika maeneo matatu ambayo ni kwenye mashamba ya kituo hicho, kwenye viwanja vya maonyesho ya wakulima (Nenenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na eneo la Igurusi wilayani Mbarali.

Dk. Bucheyeki alisema mbali na mbegu za maharage, pia wameandaa mbegu za viazi, mahindi, mpunga, ngano, soya, ulezi, maparachichi na alizeti na kwamba baadhi ya wakulima kutoka maeneo tofauti tumekuwa wakienda kujifunza mbinu bora za kilimo kwenye kituo hicho.

"Sisi kazi yetu ni kuhakikisha tunawawezesha wakulima wetu kuzalisha mazao kwa wingi na yenye ubora. Ili kufanikisha hilo ni kwamba hatuishii tu kuwafundisha bali tunaandaa na mbegu ambazo miongoni mwake ni hizi hapa," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa kwa sasa wanazalisha zaidi mbegu za mazao zenye madini ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kukabiliana na utapiamlo na udumavu ambavyo ni tatizo kubwa kwenye mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mtafiti na Mbunifu wa Mbegu za Mazao TARI Uyole, Keneth Sabula, alisema wana malengo ya kuhakikisha kila mwaka wanabuni mbegu tofauti za mazao kulingana na mahitaji ya soko pamoja na chakula kwa wananchi.

Sabula alisema moja kati ya vitu ambavyo wanawasisitiza wananchi kuvifanya ni pamoja na kuhakikisha wanapima afya ya udongo, ili wachaguwe mazao ya kupanda kwa usahihi kulingana na aina ya virutubisho vilivyomo.

Alisema kituo hicho kina maabara ambayo ina vifaa vya kutosha kwa ajili ya shughuli hiyo na baadhi ya wananchi wanaojua umuhimu wa kupima udongo wameshaanza kupeleka sampuli kwa ajili ya kupimiwa.

"Ukipita kwenye mashamba yetu yote utaona kuna aina tofauti za mazao, tunajaribu kuwaonyesha wakulima utofauti wa mbinu za uzalishaji, hapa tuna mahindi ambayo mkulima akifuata kanuni ambazo tunawaelekeza, anaweza kuvuna mpaka gunia 30," alisema Sabula.

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/9/2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/9/2020 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/6/2020 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 649 | 701 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 383 | 327 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 5,936 | 1,498 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 11,620 | 11,809 |
| 12 | Mali nyingine | 4,280 | 3,005 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 360 | 369 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **23,228** | **17,709** |
| | | | |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,010 | 15,191 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 95 | 95 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 571 | 257 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 277 | 203 |
| 28 | Madeni | 2,846 | 2,946 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **17,801** | **18,695** |
| 30 | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **5,427** | **(986)** |
| | | | |
| | | | |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | 2,764 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (4,203) | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 633 | (4,203) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 208 | 343 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | | 111 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **5,427** | **(986)** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1312 | 1011 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 520 | 563 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 23.36% | -5.57% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 11.10% | 8.17% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82.94% | 77.74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 50.03% | 66.68% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 83.39% | 85.37% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7.77% | -2.56% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 31.17% | -2.64% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30/9/2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/9/2020 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/9/2019 | Limbikizo lamwaka sasa 30/9/2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/9/2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,008 | 822 | 2,858 | 2,329 |
| 2 | Gharama za Riba | 277 | 166 | 660 | 531 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **731** | **656** | **2,198** | **1,797** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 51 | 11 | 51 | 89 |
| | | | | | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **178** | **186** | **552** | **670** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | | 0 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 137 | 140 | 410 | 396 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 41 | 46 | 142 | 274 |
| 7 | **Gharma Zisizo za Riba:** | **568** | **703** | **2,066** | **2,087** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 325 | 281 | 860 | 827 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 44 | 60 | 131 | 173 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 199 | 362 | 1,075 | 1,087 |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **291** | **128** | **633** | **292** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (58) | (26) | (127) | (58) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **233** | **102** | **507** | **234** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **233** | **128** | **633** | **292** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 56 | 47 | 56 | 47 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 8.91 | 15.69 | 19.38 | 35.80 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 36 |
| | | | | | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.42% | 0.74% | 3.09% | 1.02% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 13.10% | 4.30% | 28.53% | 9.80% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 47.87% | 69.76% | 60.58% | 73.96% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 6.13% | 3.43% | 13.35% | 8.13% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30/9/2020

| | | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | **2,764** | **-** | **(4,203)** | **24** | **87** | **-** | **(1,328)** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 633 | - | - | - | **633** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Miamala na Wanahisa | (5) | - | - | - | - | - | **(5)** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 6,127 | - | - | - | - | - | **6,127** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,886** | **-** | **(3,570)** | **24** | **87** | **-** | **5,427** |
| | | | | | | | | |
| | **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| | Salio la mwanzo wa mwaka | **2,748** | **-** | **(5,556)** | **504** | **88** | **1** | **(2,215)** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 409 | - | - | - | **409** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 944 | (480) | (1) | (1) | **462** |
| | Mengineyo | 16 | - | - | - | - | - | **16** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,764** | **-** | **(4,203)** | **24** | **87** | **(0)** | **(1,328)** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30/9/2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/9/2020 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/6/2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/9/2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/9/2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 291 | 175 | 633 | 164 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | - |
| | Hasara Katika Mali | 91 | 54 | 182 | 127 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 138 | (270) | (1,211) | 115 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,181) | 1,097 | (483) | 1,302 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | 432 | (52) | 246 | 215 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (148) | (352) | 764 | (687) |
| | Kodi Iliyolipwa | (45) | (20) | (160) | (63) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli** | **(422)** | **632** | **(29)** | **1,172** |
| | **Zauendeshaji** | | | - | |
| | | | | - | |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | - | | - | |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | - | | - | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (32) | - | (66) | (37) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | | - | - | - |
| | **(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(32)** | - | **(66)** | **(37)** |
| | | - | | - | |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (100) | (99) | (199) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | 5,000 | - | 5,000 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (5) | - | (5) | (1) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | - | - | (360) |
| | Mengineyo (bainisha) | | - | - | (89) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | **4,895** | **(99)** | **4,796** | **(450)** |
| | **Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | | | | |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | - | - | - | - |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 4,441 | 533 | 4,701 | 686 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,526 | 2,266 | 2,266 | 2,430 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **6,967** | **2,799** | **6,967** | **3,116** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

*Jina Na Cheo* *Saini* ***Tarehe***

Philipo Raymond ……………………………...….. (Imesainiwa) **27/Oct/2020**
Meneja Mkuu

Kelvin Mushi …...……………..……………... (Imesainiwa) **27/Oct/2020**
Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala

Hilda Valerian………………………………........... (Imesainiwa) **27/Oct/2020**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

**Jina** **Tarehe**

1. Prof.Domicus Kasilo………………………… (Imesainiwa) **27/Oct/2020**
Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi

2. Bw.Kitova Mungai …………………………….... (Imesainiwa) **27/Oct/2020**
Mkurugenzi

## MUCOBA BANK PLC- CHARGES AND FEES- 2020

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | | 4% |
| 6 months | | 5% |
| 12months | | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs **10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,000 |
| Cash withdrawal- (Tzs 5,000,000 and above) | Tzs 1,000 plus 0.08% of excess above 5,000,000, Max |
| | Tzs 150,000 |
| Account closure | 15,000 |
| Dormant account reactivation | 3,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,000 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Interim Statement Fee | 1,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balancy Inquiry | 100 |
| Money Transfer | 12,000 |
| ATM card replacement | 15,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 1,000 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |

# CCM yaibuka mshindi majimbo mengi




Baadhi ya wakazi wa Kata ya Nzuguni, jijini Dodoma, wakiangalia matokeo ya udiwani baada ya kubandikwa na msimamizi wa uchaguzi wa kata hiyo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeibuka mshindi katika majimbo karibu yote katika uchaguzi mkuu uliofanyika juzi.

Mpaka tunaingia mtamboni usiku wa kuamkia leo, ni jimbo moja tu ambalo upinzani ulikuwa umeambulia kati ya majimbo yote ambayo matokeo yalikuwa yametangazwa.

CCM imepoteza Jimbo la Mtwara Vijijini baada ya mgombea wake, Hawa Ghasia kupata kura 18,564 dhidi ya 26,215 za mpinzani wake, Shemsia Mtamba wa Chama cha Wananchi (CUF).

CCM pia imetangazwa mshindi katika nafasi za uwakilishi katika majimbo yote 32 ya Unguja. Matokeo yaliyokuwa yametangazwa hadi tunaingia mtamboni ni kama ifuatavyo:

### ARUSHA
### Monduli

Fredrick Lowassa wa CCM alitangazwa mshindi katika jimbo hilo baada ya kupata kura 78,307, akifuatwa na Cecilia Ndosi wa CHADEMA (4,637), Mwahija Choga wa ACT-Wazalendo (485) na Awamu Kijuu wa NRA (145).

### ARUMERU MAGHARIBI

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Gibson Blasus (CHADEMA), ameangushwa na Noah Lembris wa CCM aliyepata kura 72,160. Gibson amepata kura 22,743, akifuatwa na John kivuyo wa ACT-Wazalendo (2,492), Mohamedy Muya wa CUF (329), Loilole Wilson wa NCCR-Mageuzi (323) na Andrew Akyoo wa UPDP (169).

### Longido

Dk. Steven Kiruswa wa CCM ameibuka mshindi katika jimbo hilo kwa kura 61,885 akifuatwa na Pauline Laizer wa CHADEMA aliyepata kura 1,037, Feruz Juma wa NRA (21) na Mkadamu Abubakar wa CUF (65).

### ARUMERU MASHARIKI

Dk. John Palangyo wa CCM ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo, baada ya kumshinda mpinzani wake Rebeca Mngodo wa CHADEMA. Dk. Palangyo amepata kura 84,858 wakati Mngodo amepata kura 14,688.

### SONGWE
### Vwawa

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo baada ya kupata kura 38,226, akimzidi mpinzani wake Fanuel Mkisi wa CHADEMA (17,157).

### Mbozi

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Pascal Haonga (CHADEMA), ameanguka licha ya kugiwa kura 18,000, akimpisha George Mwanisongole wa CCM aliyepata kura 40,834. Mgombea wa CUF, Nkunyuntila Siwale amepata kura 261.

### MANYARA
### Hanang'

Samweli Hhayuma wa CCM ameshinda kuliwakilisha jimbo hilo kwa kura 50,780, akiwamwaga Derick Magoma wa CHADEMA (20,342) na Safari Mandoo wa ACT-Wazalendo (1,047).

### SHINYANGA
### Kahama Mjini

Jumanne Kishimba wa CCM ametetea kiti cha ubunge wa Kahama Mjini akipata kura 35,709 akifuatwa na Thadeo Asseche wa CHADEMA (10,740), Idsam Mapande wa ACT-Wazalendo (1,094), Mchungaji Hosea Paul wa CUF (420), Ibrahim Kwikima wa NCCR-Mageuzi (335) na Zaid Muyoba wa DP (74).

Jimbo hilo pia lina kata 20 ambazo CCM imetangazwa kushinda zote dhidi vyama saba vilivyokuwa vimesimamisha wagombea wa udiwani.

### Msalala

Idd Kassimu alitangazwa na NEC kupita bila kupigwa katika Jimbo la Msalala lenye kata 18 ambazo zote zimechukuliwa wagombea wa CCM.

### Kishapu

Boniphace Butondo wa CCM ameibuka mshindi baada ya kupigiwa kura 54,864, akimzidi Idd Amri wa CHADEMA (9,903).

### Shinyanga Mjini

Patrobas Katambi wa CCM ameibuka kidedea katika jimbo hilo kwa kura 31,831, akifuatwa na Salome Makamba wa CHADEMA (16,608), Godwin Makomba wa ACT-Wazalendo (883), Charles Shigino wa NCCR-Mageuzi (133), Abdallah Sube wa Demokrasia Makini (99), Yahya Hamisi wa UDP (69) na Malengo Elias wa TLP (63).

### MWANZA
### Ilemela

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo baada ya kupata kura 147,724, akifatwa na Grayson Warioba wa CHADEMA (24,022), Mkiwa Kimwaga (ACT-Wazalendo (2,761), Mohamed Msanya wa Demokrasia Makini (664), Shabani Itutu wa ADC (560), Ahmad Mkangwa wa NRA (218) na Clement Masonyi wa DP (102).

### Sumve

Kasalali Mageni wa CCM alitangazwa mshindi katika Jimbo la Sumve baada ya kupata kura 31,373

### Kwimba

Mansoor Jamar wa CCM ameshinda Jimbo la Kwimba baada ya kupigiwa kura 57,943.

### Sengerema

Tabasamu Mwagao wa CCM ameshinda katika jimbo hilo kwa kupata kura 59,734, akifuatwa na Victoria Tindabatangile wa CHADEMA (7,949) na Mchele Mathias wa CUF (497).

### Misungwi

Alexander Mnyeti wa CCM alitangazwa na NEC kupita bila kupigwa katika jimbo hilo lililowakilishwa na Charles Kitwanga Bunge la 11.

### SIMIYU
### Kisesa

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ameshina tena ubunge wa Kisesa akipata kura kura 18,335 dhidi ya 14,944 za mgombea wa CHADEMA.

### Busega

Simon Lusengekile wa CCM ametangazwa mshindi katika jimbo hilo kwa kupata kura 35,770 akifuatwa na Alphonce Komanya wa CHADEMA (9,063).

### Meatu

Mshindi katika jimbo hilo ni Leah Komanya wa CCM aliyepata kura 16,239 dhidi ya mpinzani wake, Johstone Luzibukya wa CHADEMA aliyepigiwa kura 14,750.

### KATAVI
### Mpanda Mjini

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mpanda Mjini, Michael Nzyungu, alimtangaza Sebastian Kapufi wa CCM kushinda kwa kura 24,020 (asilimia 63.4), akifuatwa na Rhoda Kunchela (CHADEMA) kura 13,611 (asilimia 35.6), Stanslaus Kisesa (ACT) kura 289 na Aron Ndimubenya (CUF) kura 66.

### Mpanda Vijijini

Selemani Kakoso wa CCM ameshinda Ubunge wa Mpanda Vijijini baada ya kupigiwa kura 35,092 akifuatiwa na Emmanuel Lusambo wa CHADEMA (5,350), Juliana Mwakangwali wa ACT-Wazalendo (2,841) na Mariam Mabuga wa NCCR-Mageuzi (237).

### Nsimbo

Anna Lupembe wa CCM ametangazwa mshindi kwa kura 38,346, akiwazidi nguvu Marystella Mallac wa ACT (1,292), Shambwe Mkasu wa CHAUMMA (1,159) na Iddi Faraji wa CHADEMA (904).

### Kavuu

Geophrey Pinda wa CCM ameshinda kwa kupata kura 41,401 akifuatiwa na Mbiti Hoga Bukelebe wa CHADEMA aliyepigiwa kura 2,920.

### MARA
### Tarime Vijijini

Mwita Waitara wa CCM ameshinda katika Jimbo la Tarime Vijijini kwa 35,758 dhidi ya 18,757 za John Heche wa CHADEMA na 941 za Charles Meera wa ACT-Wazalendo.

### Tarime Mjini

Kembaki wa CCM ametangazwa mshindi kwa kura 18,235 akimng'oa Esther Matiko wa CHADEMA aliyepata kura 10,873. Katika uchaguzi huo, Ryoba Magwi wa ACT-Wazalendo amepata kura 265, Tangori Zacharia (CUF) kura 43 Elias Nyagabona wa NCCR-Mageuzi kura 143 na Wambura Chacha wa SAU kura 42.

### KILIMANJARO
### Moshi Mjini

Hatimaye CCM imeshinda kwa mara ya kwanza kiti cha ubunge wa Moshi Mjini baada ya jimbo hilo kushikiliwa na upinzani kwa miaka 25. Priscus Tarimo wa CCM alitangazwa mshindi jana akimwangusha mpinzani wake, Raymond Mboya (CHADEMA) kwa tofauti ya kura 8,614.

Tarimo amepata kura 31,169, akifuatwa na Mboya (22,555), Abdul Ramole wa ACT-Wazalendo (374), Isaac Kimaro wa SAU (93), Fatma Msuya wa CUF (85), Mchungaji Dk. Godfrey Malisa wa NCCR-Mageuzi (59) na Neema Mushi wa Demokrasia Makini (51).

### HAI

Freeman Mbowe, ameshindwa kutetea Jimbo la Hai alilolingoza kwa miaka 10 mfululizo, akiangushwa na Saashisha Mafuwe (CCM) aliyepata 89,786 dhidi ya 27,684 za Mwenyekiti huyo wa CHADEMA 305 za Mbarouk Mhina (ACT-Wazalendo).

### Siha

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ametetea kiti cha Ubunge wa Siha, akipata kura 22,172 dhidi ya 8,614 za mpinzani wake wa siku nyingi, Elvis Mossi (CHADEMA).

Wagombea wengine katika jimbo hilo ni Leslie Kileo (NCCR-Mageuzi) aliyepata kura 306 na Amedeus Kitali (ACT-Wazalendo) kura 418.

INAENDELEA UK. 19

# CCM yaibuka mshindi majimbo mengi

INATOKA UK. 18

**Rombo**

Profesa Adolf Mkenda ameshinda Ubunge wa Rombo kwa kura 48,122 dhidi ya Patrick Assenga (CHADEMA) aliyepata kura 9,519, Japhet Masawe wa ACT-Wazalendo (1,564), Joseph Selasini wa NCCR-Mageuzi (416) na Michael Kimaro wa TLP (167).

**TANGA**
**Korogwe Mjini**

Katika Jimbo la Korogwe Mji mkoani Tanga, Alfred Kimea wa CCM alitangazwa mshindi baada ya kupata kura 16,969, akiwabwaga Winjones Clerente (CHADEMA) aliyepata kura 2,116, Amina Magogo (CUF) kura 1,497 na Bahati Chirwa (ACT-Wazalendo) kura 304.

**Mlalo**

Rashid Shangazi wa CCM amechaguliwa tena kuwa mbunge wa jimbo hilo kwa kura 46,632, akiwashinda Amir Mohamed wa CHADEMA (2,803) na Laurant Mnkai wa ACT- Wazalendo (1,671).

**Handeni**

CCM pia imeshinda ubunge wa Handeni kupitia mgombea wake, Reuben Kwagilwa, aliyepata kura 15,241 akifuatwa na Sonia Magogo wa CUF, aliyepigiwa kura 6,114.

**Lushoto**

Shaaban Shekilindi wa CCM ameshinda tena ubunge wa jimbo hilo kwa kura 20,799, akiwazidi Walter Mbelwa wa CHADEMA (4,086) na Athuman Dhahabu wa ACT-Wazalendo (1,163).

**Tanga Mjini**

Ummy Mwalimu (CCM) ameshinda ubunge wa jimbo hilo baada ya kupata kura 114,445, akimng'oa aliyekuwa mbunge wake, Mussa Mbarouk, aliyepata kura 7,497. Pia kata zote 27 za jimbo hilo zimechukuliwa na CCM.

**Kilindi**

Omar Kigua wa CCM ametetea kiti chake katika jimbo hilo akimbwaga mpinzani wake, Maimuna Said wa ADC.

**MTWARA**
**Nanyamba**

Abdallah Chikota wa CCM ameshinda kwa kura 22,262, akifuatwa na Mohamed Hassan Ndaile wa CUF (11,265), Dadi Mayenda wa CHADEMA (2,024), Colleta Kandida wa ACT-Wazalendo (755) na Asia Namava wa NCCR-Mageuzi (269).

**Mtwara Vijijini**

Ghasia wa CCM ameshindwa kutetea jimbo hilo, akiangushwa na Mtamba wa CUF. Wagombea wengine katika jimbo hilo na kura zao kwenye mabano ni Fuata Issa wa ACT (1,372), Mtuma Yusufu wa CHADEMA (1,020) na Ismail Mohamed wa NCCR-Mageuzi (207).

**TABORA**
**Nzega Mjini**

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ametetea kiti cha Ubunge wa Nzega Mjini kwa kura 16,082 dhidi ya 2,663 za Maria Atonga wa CHADEMA, 166 za Antony Sambali wa ACT-Wazalendo na 102 za Masoud Salumu wa CUF.



Mgombea ubunge katika Jimbo la Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), akifurahia ushindi pamoja na wanachama wenzake baada ya kutangazwa mshindi wa jimbo hilo, na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, Hamid Njovu (kulia) jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

**Kaliua**

Aloyce Kwezi wa CCM amepata kura 35,065 na kumng'oa Magdalena Sakaya wa CUF katika jimbo hilo. Sakaya amepata kura 8,187 akifuatwa na Samson Balazingiza wa CHADEMA (1,295).

**Nzega Vijijini**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, alitangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupita bila kupingwa katika Jimbo la Nzega Mjini.

**KIGOMA**
**Muhambwe**

Atashasta Nditiye wa CCM amepata kura 29,837 akifuatwa na Felix Mkosamali wa CHADEMA (15,248), Julius Masabo wa ACT (2,996) na Nicholaus Kirunga wa CUF (473).

**MOROGORO**
**Morogoro Mjini**

Abdul-Aziz Abood ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo baada ya kupata kura 171,339, akiwabwaga Hussein Sheshe wa ACT (720), Devotha Minja wa CHADEMA (14,139) na Abeid Mlapakolo wa CUF (562).

**Kilosa**

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alishatangazwa na NEC kupita bila kupigwa.

Wabunge wateule wengine walionufaika na utaratibu huo katika Mkoa wa Morogoro ni Jonas Van Zeeland (Mvomero), Kalogereris Innocent (Morogoro Kusini) na Taletale Shabani (Morogoro Mashariki).

**Ulanga**

Salim Hasham wa CCM ameshinda kwa kura 32,613 dhidi ya Selestine Emanuel wa CHADEMA (9,393) na Batuli Mtenga wa CUF (459).

**Mikumi**

Dennis Londo wa CCM ameshinda ubunge wa jimbo hilo kwa kupigiwa kura 31,411 dhidi ya aliyekuwa mbunge wake, Joseph Haule 'Profesa Jay' wa CHADEMA aliyepata kura 17,375.

**MBEYA**
**Mbeya Mjini**

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameweka rekodi ya kuwa mbunge wa kwanza mwanamke katika Jimbo la Mbeya Mjini akimwangusha Joseph Mbilinyi 'Sugu' baada ya kupata kura 75,225 dhidi ya 37,591 za mgombea huyo wa CHADEMA.

**Mbarali**

Francis Mtega wa CCM ameshinda ubunge wa jimbo hilo kwa kura 55,737, akifuatwa na Liberatus Mwang'ombe wa CHADEMA (28,104), Juma Haji wa ACT-Wazalendo (1,256) na Zavery Laurent wa UDP (338).

**DAR ES SALAAM**
**Kinondoni**

Abass Tarimba wa CCM ameshinda kwa kura 112,014, akifuatwa na Susan Lymo wa CHADEMA (11,260), Saed Kubenea wa ACT-Wazalendo (5,946) na Salum Juma wa CUF (5,948).

**GEITA**
**Geita Mjini**

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu ameshinda tena ubunge wa Geita Mjini kwa kura 30,277 akifuatwa na Upendo Peneza wa CHADEMA (17,272), Emmanuel Otto wa ACT-Wazalendo (260), Francis Mahenge wa CCK (245), Michael Peter wa CUF (101) na Wilbert Maganga wa NCCR-Mageuzi (50).

**SINGIDA**
**Singida Mashariki**

Miraji Mataturu ametetea tena kiti cha ubunge wa jimbo hilo kwa kura 25,913, akimshinda Hemed Kurungu wa CHADEMA aliyepigiwa kura 16,546.

**Singida Magharibi**

Elibariki Kingu wa CCM ameshinda tena ubunge wa jimbo hilo baada ya kupigiwa kura 32,450 dhidi ya 7,650 za mpinzani wake, Hemedi Ramadhani (CHADEMA).

**KAGERA**
**Nkenge**

Innocent Kyombo wa CCM ameshinda ubunge wa Nkenge kwa kura 58,051, akiwazidi kete Magreth Kyai wa CHADEMA (4,803) na Leonard Kabaka wa ACT-Wazalendo (621).

**Bukoba Mjini**

Steven Byabato wa CCM ametangazwa mshindi katika jimbo hilo kwa kura 29,883, akimzidi kete Chief Kalumuna wa CHADEMA aliyepata kura 16,673.

**DODOMA**
**Bahi**

Keneth Nollo wa CCM ameibuka kidedea kwa kura 40,629 huku mgombea wa CUF, Godfrey Pamwe, akipata kura 2,254.

**ZANZIBAR**

Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imetangaza matokeo ya uwakilishi na udiwani, huku majimbo yote 32 ya Unguja yakichukuliwa na CCM kwa nafasi ya uwakilishi.

**Donge**

Dk. Khalid Salum Mohammed, amepata kura 9,696 dhidi ya mpinzani wake Pavu Juma wa ACT-Wazalendo aliyepata kura 501.

**Mahonda**

Asha Abdalla Mussa wa CCM amepata kura 9,729, akifuatwa na Thuwaiba Juma Hassan wa ACT-Wazalendo (1,349) na Tajo Khamis Omar wa CHADEMA (1,092).

**Bumbwini**

Mtumwa Peya Yussuf wa CCM amepata kura 10,348 na kuwapita wapinzani wake, Zuhura Juma wa ACT-Wazalendo (2,410) na Abdallah Ali Ameir wa CUF (169).

**Chaani**

Mshindi wa Uwakilishi kwenye jimbo hilo ni Nadir Abdu-latif Yussuf wa CCM aliyepata kura 10,197, akimshinda mpinzani wake Khamis Ali Juma wa ACT-Wazalendo aliyeambulia kura 1,055.

**Nungwi**

Katika jimbo hilo, aliyeshinda ni Abdallah Abass wa CCM aliyepata kura 7,513 akifuatiwa na Khamis Juma Shomar wa CHADEMA (2,378) na Juma Simai Omar wa CUF (1,016).

**Tumbatu**

Mwakilishi pekee wa jimbo hilo alikuwa ni Haji Omar Kheir aliyepita bila ya kupingwa pamoja na diwani wake, wote kutoka CCM.

**Kijini**

Aliyeshinda nafasi ya uwakilishi katika jimbo hilo ni Juma Makungu Juma wa CCM aliyepata kura 6,957 na kumshinda Asha Abdalla Ramadhan wa CUF aliyepata kura 1,826.

**Uzini**

Aliyeshinda nafasi hiyo ni Haji Shaaban Wazir kutoka CCM aliyepata kura 16,276 na mpinzani wake kutoka ACT-Wazalendo, Hamran Naimu Membar, amepata kura 990.

**Chwaka**

Mshindi wa uwakilishi ni Issa Haji Gavu wa CCM ambaye amepata kura 9,302 na kumshinda mpinzani wake aliyepata kura 1,133 wa ACT-Wazalendo.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR), Godfrey Mushi (SIHA), Lulu George (TANGA), Shaban Njia (KAHAMA), Neema Hussein (KATAVI), Marco Maduhu (SHINYANGA), Edwin Katonga (NZEGA), Mary Mosha (ROMBO), Boniface Gideon (HANDENI), Allan Isack (MONDULI), Rahma Suleiman (ZANZIBAR), Hamisi Nasri (NAMNYAMBA), Woinde Shizza (ARUMERU), Neema Emmanuel na Richard Makore (MWANZA).***

# MESSI NI 'HARRY POTTER' WA SOKA – VIERI




**TURIN,** Italia

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi ni "Harry Potter" wa soka, kwa mujibu wa Christian Vieri.

Harry Potter ni mfululizo wa hadithi na filamu maarufu zaidi duniani kutoka nchini Uingereza zilizotungwa na mwanamama J. K. Rowling.

Messi alitoa pasi ya mwisho kwa Ousmane Dembele aliyefunga bao la ufunguzi kabla ya yeye kufunga kwa penalti dakika za majeruhi wakati Barcelona wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Juventus kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alikuwa na mchango mkubwa kwenye mchezo huo akipiga pasi muhimu tano na pasi nyingine 65, wakati Barca ikionekana kuimarika zaidi na kupata pointi sita kwenye Kundi G.

Vieri, ambaye alishinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Juve msimu wa 1996-97 na alikuwa na mabao 49 kwenye Timu ya Taifa ya Italia, amesifia mchango wa Messi kwenye mchezo huo uliopigwa hapa Turin.

"Ni Barcelona ya kuvutia, ulikuwa mchezo mzuri. Wangeweza kufunga mabao sita au saba kiurahisi. Walicheza soka la kuvutia sana," alisema Vieri akiiambia CBS Sports.

"Messi ni mtu wa miujiza, yeye ni Harry Potter wa soka na wakati atakapoacha kucheza nitaitupa televisheni yangu.

# Pirlo: Juve lazima ishinde huku ikijengwa

**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo amesisitiza msimu huu hautakuwa wa mpito kirahisi kwa Juventus, akisema anataka kushinda.

Baada ya ushindi mara mbili kwenye mechi tano za ufunguzi wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juve ilikumbana na kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Pirlo, ambaye alichukua nafasi ya ukocha Agosti, amesema wakati miamba hao wa Italia wakijijenga upya, bado anataka ushindi.

"Hapana, ni mwaka ambao tunajijenga upya, lakini tunataka kujaribu kupata matokeo. Siko hapa kwa ajili ya kucheza bila ushindi," alisema kocha huyo wa Juve akiwaambia waandishi wa habari.

"Pengine tutahitaji muda zaidi, lakini tunatakiwa kujua matokeo yanakuja kwanza bila kujali tunacheza kwa staili gani."

Mabao kutoka kwa Ousmane Dembele ana Lionel Messi huku Merih Demiral akilimwa kadi nyekundu, yalishuhudia Barca ikiibuka na ushindi pale Turin.

Mshambuliaji wa Juve, Alvaro Morata alionyesha kucheza kwa kiwango cha juu na alikuwa tishio kwa safu ya ulinzi ya Barcelona.





# Koeman hana hofu na nafasi yake

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman ana matumaini angeambiwa kama kuna mabadiliko kwa upande wake pale Barcelona baada ya kujiuzulu kwa Rais, Josep Maria Bartomeu.

Siku moja baada ya Bartomeu kujiuzulu, Barca walionyesha kiwango cha kuvutia wakati wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kukosa kutwaa taji lolote msimu wa 2019-20, Koeman aliteuliwa kuwa kocha mpya wa Barca Agosti, na miamba hao wa LaLiga walikuwa kwenye wakati mgumu wa kumtuliza Lionel Messi ambaye aliomba kuondoka, kabla ya kuamua kubaki.

Alipoulizwa kama anahofia nafasi yake baada ya kujiuzulu kwa Bartomeu, Koeman alisema hilo sio tatizo kwake.

"Hapana. Tuna nguvu ya kucheza soka tu kwa sasa. Mambo ya nje ya uwanja yapo nje ya uwezo wangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa hali yangu kubadilika kwa namna yoyote, natumaini ningeambiwa kuhusu hilo. Tunataka kupata matokeo bora na kuimarika kwa uchezaji.

"Hilo ndilo ambalo kwa sasa tunaliangalia kwa upande wetu. Kitu kingine chochote nje ya hayo sio majukumu yetu. Tutaona nini kitatokea.

"Sihusiki sana na kile kinachotokea nje ya uwanja. Sisi akili yetu ni kile kinachotokea uwanjani."

TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|
| **A .** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,837 | 5,522 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 397,112 | 100,542 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 123,932 | 155,322 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 846,158 | 345,468 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 86 | 230 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 12,225 | 4,915 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 26,154 | 15,235 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 319,804 | 359,459 |
| 12 | Mali Nyingine | 7,049 | 6,626 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,336 | 9,183 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **1,746,693** | **1,002,502** |
| **B .** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 948 | 21,741 |
| 18 | Amana za Wateja | 1,593,882 | 838,765 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 7,573 | 7,567 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,660 | 2,594 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,584 | 3,878 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 26,210 | 15,274 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 408 | 417 |
| 27 | Dhima Nyingine | 14,243 | 16,505 |
| 28 | Madeni | 0 | 0 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **1,650,508** | **906,741** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** | **96,185** | **95,761** |
| **C .** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 | - Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | - Mapato Yaliyobakizwa | 80,820 | 81,247 |
| 34 | - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,571 | 1,753 |
| 35 | - Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,134 | 3,101 |
| 36 | - Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **96,185** | **95,761** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 141,270 | 110,273 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 0 | 0 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,266 | 1,402 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| **D .** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 5.5% | 9.6% |
| ( ii ) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 20.0% | 41.4% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 18.3% | 35.9% |
| ( v ) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73.8% | 85.8% |
| ( vi ) | Ongezeko la Amana | 45.8% | -8.7% |
| ( vii ) | Ongezeko la Mali | 42.6% | -9.1% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 7,311 | 8,715 | 24,517 | 25,699 |
| 2 | Gharama za Riba | (3,692) | (3,085) | (9,828) | (7,642) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba** | **3,619** | **5,630** | **14,689** | **18,057** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 135 | (280) | (467) | (498) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,272** | **4,370** | **9,514** | **14,040** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2,216 | 2,216 | 6,040 | 8,034 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,056 | 2,154 | 3,474 | 6,006 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,875)** | **(5,715)** | **(18,718)** | **(19,053)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,688) | (1,864) | (5,646) | (7,811) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,187) | (3,851) | (13,072) | (11,242) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,151** | **4,005** | **5,018** | **12,546** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (337) | (689) | (2,447) | (3,579) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **814** | **3,316** | **2,571** | **8,967** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| | Mapato ambayo hayajakamilika | (563) | 246 | (120) | (425) |
| | Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 169 | (74) | 36 | 127 |
| | Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | (394) | 172 | (84) | (298) |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **420** | **3,488** | **2,487** | **8,669** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 44 | 45 | 44 | 45 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 81,435 | 331,633 | 257,070 | 896,749 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D .** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.2% | 1.5% | 0.3% | 1.3% |
| ( ii ) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.4% | 13.1% | 3.5% | 11.9% |
| ( iii ) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 55.5% | 43.7% | 55.0% | 47.9% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.1% | 5.7% | 4.1% | 6.1% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) — Date : 27 Octoba 2020

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) — Date : 27 Octoba 2020

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) — Date : 27 Octoba 2020

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Emilian Busara — Date : 27 Octoba 2020

Imesainiwa na: Yande Panya — Date : 27 Octoba 2020

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,151 | 554 | 5,018 | 12,546 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | -Hasara Katika Mali | 460 | 762 | 1,501 | 122 |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 39,655 | (24,469) | (26,369) | (102,592) |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 734,324 | (75,231) | 866,128 | (86,058) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 9,444 | (16,142) | 9,835 | (17,024) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (17,908) | 21,664 | (13,114) | 15,158 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (801) | (801) | (2,703) | (4,487) |
| | -Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **766,325** | **(93,663)** | **840,296** | **(182,335)** |
| **II .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (718) | (1,835) | (2,761) | (177) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 30,826 | 1,977 | 31,680 | 4,166 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **30,108** | **142** | **28,919** | **3,989** |
| **III .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | (12,000) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **0** | **0** | **0** | **(12,000)** |
| | | **796,433** | **(93,521)** | **869,215** | **(190,346)** |
| **IV .** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **796,433** | **(93,521)** | **869,215** | **(190,346)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 451,761 | 545,282 | 378,979 | 541,721 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,248,194 | 451,761 | 1,248,194 | 351,375 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **92,611** | **0** | **0** | **1,597** | **103,868** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 1,753 | 0 | 0 | 0 | **1,753** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 310 | **310** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (10,170) | 0 | 0 | 0 | **(10,170)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,194) | 1,194 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **83,000** | **1,194** | **0** | **1,907** | **95,761** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **92,054** | **0** | **2,387** | **1,148** | **105,249** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 5,651 | 0 | 0 | 0 | **5,651** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | (471) | **(471)** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (12,061) | 0 | 0 | 0 | **(12,061)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (2,026) | 0 | 2,026 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **83,618** | **0** | **4,413** | **677** | **98,367** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

### CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

| 1.0 | Current Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|---|
| | (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| | (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| | (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| | (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| | (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| | (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| | (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| | (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| | (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| | (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| | (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 4.55%-7.80% | 1.59%-7.34% |
| | (r) Unarranged overdraft | 23.00% | 14% |
| | (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| | (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| | (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| | (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| | (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| | (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| | (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| | (b) Monthly service fee | NA | NA |
| | (c) Interim statement | NA | NA |
| | (d) Account clossure | NA | NA |
| **3.0** | **Electronic Banking** | | |
| | (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| | (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 |
| | (c) SMS banking | N/A | N/A |
| | (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

| 4.0 | Foreign Exchange Transactions | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|---|
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| | (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| | (d) Telegraphic transfer | | |
| | -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| | -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| | (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |
| **5.0** | **Personal Loans** | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| | (i) Personal loans | NA | NA |
| | (ii) Overdrafts | NA | NA |
| | (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| | (iv) Asset finance | NA | NA |
| | (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| | (c) Early repayment | NA | NA |
| | (d) Valuation fees | NA | NA |
| | (e) Other | NA | NA |

**Additional Disclossures**

| 1 | Deposit Rates | LCY | FCY |
|---|---|---|---|
| | -Current Account Deposits | 0%-5.00% | 0%-0% |
| | -Time Deposits | | |
| | (a) 1 - Months | 1.79% -1.99% | 0.13%-0.14% |
| | (b) 3 - Months | 2.12% -2.42% | 0.21%-0.23% |
| | (c) 6 - Months | 2.28% -2.58% | 0.22%-0.24% |
| | (d) 9 - Months | 3.96% -3.26% | 0.27%-0.30% |
| | (e) 12 - Months | 3.63% -3.93% | 0.32%-0.36% |
| **2** | **Lending Rate** | **LCY** | **FCY** |
| | Base lending rate | 5.08%-6.08% | 2.71%-3.71% |
| | Short term ( up to one year ) | 5.08%-6.08% | 2.71%-3.71% |
| | Medium term ( 2 to 3 years ) | 5.58%-6.58% | 3.21%-4.21% |
| | Long term ( 3 - 5 years ) | 6.08%-7.08% | 3.71%-4.71% |
| | Term loans ( over 5 years ) | 6.08%-7.08% | 3.71%-4.71% |

| 6.0 | Trade Finance | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| | **Documentary Collections** | |
| | Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| | Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| | **Imports Letters of Credits** | |
| | Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| | Handling fees | Handling: $130 |
| | Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| | Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| | Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| | Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | **Exports Letters of Credits** | |
| | Handling fees | $500 |
| | Courier | $100 |
| | Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| | **Liquidity financing** | |
| | Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| | SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| | Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | Name | Designation | | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................ | Date : 27th October 2020 |
| 2 | Leila Senkoro | Acting TTS Head | ........................................................ | Date : 27th October 2020 |
| 3 | James Rutta | Head of Treasury | ........................................................ | Date : 27th October 2020 |

# MAKALA YA MAFANIKIO YALIYOFIKIWA NA TAASISI YA KUTHIBITI UBORA WA MBEGU TANZANIA (TOSCI) KATIKA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO (2015-2020) CHINI YA UONGOZI WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA Mhe. Dkt. JOHN POMBE MAGUFULI

Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Kilimo na ilianzishwa kwa Sheria ya Mbegu Namba 18 ya Mwaka 2003. TOSCI ilichukua nafasi ya Wakala wa Taifa wa Kuthibiti Ubora wa Mbegu (Tanzania Official Seed Certification Agency-TOSCA) iliyoanzishwa mwaka 1973. Taasisi inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye pia ni Mthibiti Mkuu wa Mbegu na ina vituo vinne vya kanda na Makao Makuu yake yapo Morogoro.

**1.0 MAJUKUMU YA TOSCI**

- Kusajili wafanyabiashara/wazalishaji wa mbegu
- Kufanya majaribio ya Utambuzi (DUS Test) na umahili wa aina mpya za mbegu (NPT)




Kielelezo Na. 1. Majaribio ya utambuzi wa aina mpya za mbegu TOSCI Makao Makuu-Morogoro



Kielelezo Na. 2. Jaribio la umahiri wa aina mpya za mbegu mkoani Iringa

- Kusajili aina mpya za mbegu
- Kusajili na kukagua mashamba ya mbegu



Kielelezo Na. 3. Wakaguzi wa mbegu wa TOSCI wakikagua shamba la mpunga wilaya ya Kilosa Morogoro

- Kuchukua sampuli za mbegu na kuzifanyia vipimo vya ubora



Kielelezo Na. 4. Mafunzo kwa Vitendo ya Uchukuaji Sampuli Wakati wa Mafunzo ya ISTA

- Kukagua maghala na maduka ya mbegu



Kielelezo Na. 5. Mkaguzi wa mbegu wa TOSCI akikagua maduka ya mbegu kanda ya Kusini, Disemba 2019

- Kutoa vibali vya kuuza/kuagiza mbegu nje ya nchi
- Kuendesha majaribio ya kuthibiti ubora wa mbegu kupitia ploti za udhibiti



Kielelezo Na. 6. Jaribio la kutathmini ubora wa mbegu za Mahindi zilizo katika uzalishaji (Control Plot Test)

- Kusimamia mfumo wa uzalishaji mbegu bora katika ngazi ya wakulima (QDS)
- Kuiwakilisha Tanzania katika majukwaa ya mbegu kikanda na kimataifa

**2.0 MAFANIKIO YA TOSCI KATI YA MWAKA 2015 NA 2020**

**2.1 Kuongezeka kwa upatikanaji na matumizi ya mbegu zenye ubora**

Wizara ya Kilimo kupitia TOSCI na kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kuimarisha upatikanaji, utumiaji na udhibiti wa ubora wa mbegu ili kuongeza tija, kipato kwa wakulima na usalama wa chakula na lishe. Kutokana na kukua kwa tasnia ya mbegu nchini, matumizi ya mbegu bora zilizothibitishwa na TOSCI yameongezeka kutoka tani 10,946 (2014/2015) hadi tani 76,285 (2019/2020). Hili ni ongezeko la asilima 86.8. Katika juhudi hizo za kuongeza matumizi ya mbegu bora, Wizara kupitia TOSCI imeongeza kiasi cha mbegu bora zilizothibitishwa zinazozalishwa hapa nchini kutoka tani 4,337 (2014/2015) hadi tani 64,304.7 (2019/2020) ambazo ni asilimia 84 ya mbegu zote zilizothibitishwa. Kwasasa mbegu bora zinazotoka nje ya nchi ni asilimia 16 tu.

**Sababu zilizochangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu nchini**

- **Uwepo wa mazingira mazuri ya wawekezaji kwenye tasnia ya mbegu**
  Kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu ni matokea ya juhudi za serikali za kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ambapo uwekezaji katika tasnia ya mbegu kumechangia kuongezeka kwa eneo linalozalishia mbegu kutoka hekta 10,674 mwaka 2014/2015 hadi hekta 99,885 mwaka 2019/2020 (Kielelezo Na. 7).

# TOLEO MAALUMU




**Kielelezo Na.7. Eneo lililotumika kuzalishia mbegu na kiasi cha mbegu kilichozalishwa nchini pamoja na kiasi cha mbegu kilicho agizwa na kuuzwa nje ya nchi kati ya mwaka wa fedha 2014/2015 na 2019/2020**

- **Uimarishwaji wa utafiti na udhibiti wa aina mpya za mbegu**
  Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI) na makampuni ya mbegu vimeimarisha shughuli za utafiti wa aina mpya za mbegu hivyo kuwezesha kupatikana kwa aina za mbegu ambazo zinatoa mavuno mengi na zinavumilia ukame, magonjwa na wadudu. Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Nchini (TOSCI) imeimarisha shughuli za majaribio ya Utambuzi na Umahiri wa aina mpya za mbegu hivyo kuhakikisha kuwa aina zote za mbegu zinazodhibitishwa na TOSCI zinakuwa na vigezo vyote muhimu kabla hazijasajiliwa. Kutokana na juhudi hizo aina mpya za mbegu zilizosajiliwazimeongezeka kutoka aina 431 (2015/2016) hadi aina 604 (2019/2020).
- **Kupungua kwa tatizo la mbegu feki**
  Moja ya changamoto kubwa iliyokuwainatishia ustawi wa tasnia ya mbegu nchini ni uwepo wa mbegu bandia (mbegu feki) hapa na pale. Katika kukabiliana na tatizo hili, TOSCI ilichukua hatua mbali mbali ambazo zimeonyesha matokeo chanya kwa kupunguza matukio ya mbegu feki kutoka 327 (2014/2015) hadi 5 (2019/2020). (Kielelezo Na. 8).




Kielelezo Na. 8. Kupungua kwa matukio ya mbegu feki/dhaifu kufuatia kuongezeka kwa matumizi ya lebo za TOSCI

**Mikakati mbali mbali inayotumiwa na TOSCI kukabiliana na tatizo la mbegu feki**

➢ **Matumizi ya lebo za TOSCI**

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na udhibiti wa ubora wa mbegu, Wizara kupitia TOSCI imekuwa ikiongeza matumizi ya lebo za ubora za TOSCI. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya lebo 9,000,000 zilitolewa na TOSCI kwa wazalishaji mbali mbali wa mbegu ikilinganishwa na lebo 400 zilizotolewa mwaka wa fedha 2014/2015. Hata hivyo ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara ya mbegu wasio waaminifu hawaingizi sokoni mbegu feki, taasisi za TOSCI na TTCL zimebuni mfumo wa kielektroniki utakao wawezesha wakulima kubaini mbegu feki zilizo na lebo feki. Kutokana na juhudi hizo matukio ya wauza mbegu kuuza mbegu feki au zisizo na viwango yamepungua kwa kiasi kikubwa. Watu wengi sasa wanapendelea kununua mbegu zenye lebo ya TOSCI ambazo zimeonekana kuwa na ubora wa hali ya juu ikilinganishwa na mbegu ambazo hazina lebo ya TOSCI.

➢ **Kutoa elimu kwa umma**

Kutoa elimu kwa wakulima na umma juu ya utambuzi wa mbegu feki kwa kupitia magazeti, redio, Runinga, semina, warsha na mikutano mbali mbali.

➢ **Kuimarisha shughuli za ukaguzi wa maghala na maduka**

Kufanya ukaguzi wa maduka yanayouza mbegu mara kwa mara, hasa wakati wa msimu wa kilimo. TOSCI imepanua wigo wa ukaguzi wa maduka yanayouza pembejeo mbegu ili kuhakikisha kuwa wauzaji wote wa mbegu wanafuata sheria na kanuni za mbegu hivyo kuuza mbegu zilizo na ubora unaotakiwa.

➢ Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara ya mbegu wote wanasajiliwa kabla ya kuanza biashara

Tangu TOSCI imepewa jukumu la kusajili wauzaji wa mbegu baada ya mabadiliko ya sheria ya mbegu ya mwaka 2014, Taasisi inahakikisha kuwa wafanyabiashara wa mbegu wanauza mbegu hizo baada ya kukidhi vigezo vya TOSCI (kupata mafunzo ya masuala ya mbegu pamoja na sheria na kanuni za mbegu, kuwa na leseni ya biashara pamoja na kuwa na TIN). Baada ya kukidhi vigezo hivi mfanyabiashara wa mbegu hupewa cheti cha usajili cha TOSCI hivyo kuwa na haki ya kuuza mbegu. Lengo la TOSCI ni kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wa mbegu wanasajiliwa na wanafuata sheria na kanuni za mbegu. Wafanyabiashara wote wa ambao wanakiuka miongozo ya sheria na kanuni za mbegu hufutiwa leseni zao za biashara ya mbegu pamoja na kufunguliwa mashitaka mahakamani.

➢ **Kuwatumia kwa ufanisi wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa na TOSCI**

Kutokana na changamoto ya kuwa na wakaguzi wa mbegu wachache wa TOSCI, taasisi iliandaa mpango mkakati wa miaka mitano (2017/2018 mpaka 2021/2022) wa kutoa mafunzo kwa Maafisa Kilimo wa Wilaya na kuwasajili ili waweze kusaidia katika kusimamia ubora wa mbegu katika maeneo yao kwa niaba ya TOSCI. Mpaka sasa tumekwisha idhinisha wakaguzi 160 kati ya 400 wanaohitajika.

➢ Kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi

Lengo ni kuhakikisha mbegu zote kutoka nje zinapewa vibali na TOSCI na kuhakikisha zinafuatiliwa kuona kama zimekidhi vigezo vya ubora vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria ya mbegu.

**2.2 Tanzania ni mwanachama wa Jumuia mbali mbali za Kimataifa zinazoshughulikia Ubora wa mbegu**

➢ **Tanzania kupata Ithibati ya " International Seed Testing Association -ISTA" (Maabara ya Mbegu ya Taifa-Morogoro)**



**Kielelezo Na. 9. Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI Ndugu Patrick Ngwediagi Akishuhudia Ukaguzi wa ISTA Katika Sehemu ya Uchambuzi wa Usafi wa Mbegu (Seed Purity Analysis)**

**Faida za kupata ithibati kutoka ISTA**

a) Kupata miongozo mbalimbali ya msingi kuhusu kanuni na taratibu za kupima ubora wa mbegu maabara
b) Kupanua wigo wa ushirikiano kati ya watafiti wa mbegu na wanasayansi ya mbegu duniani
c) Kuhakikishia ulimwengu juu ya mifumo linganifu ya upimaji ubora wa mbegu maabara kupitia miongozo na mitihani ya kitaalamu kwa maabara za nchi wanachama.
d) Kupata mafunzo ya kuongeza ujuzi na maarifa kwa wafanyakazi wa maabara kimataifa
e) Kutetea maslahi ya mbegu kwa kupaza sauti ya pamoja isiyobagua juu ya sekta ya mbegu duniani

➢ Tanzania kujiunga na Skimu za Mbegu za Shirika la Kimataifa la Organization for Economic Cooperation and Development Seed Schemes- OECD Seed Schemes)

**Faida za kujiunga na skimu za mbegu za OECD ni:**

a) Kusaidia kufanikisha biashara ya kimataifa ya mbegu kwa kuunganisha taratibu na mbinu za uthibiti ubora wa mbegu, kufanya ukaguzi wa mashamba na kuanzisha vishamba vya majaribio kwa nchi wanachama. Pia kuongeza utambuzi wa uhalisia wa aina mpya za mbegu kulingana na viwango vya nchi wanachama
b) Kutengeneza miongozo ya uzalishaji wa mbegu kwa mataifa na makampuni ya mbegu
c) Kushiriki katika kuelezea na kutoa ufafanuzi wa sheria za kimataifa za uthibiti ubora wa mbegu
d) Kuhamasisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika masuala ya mbegu
e) Kuimarisha ushirikiano katika kubadilishana taarifa na ujuzi na taasisi nyingine za uthibiti ubora wa mbegu za nchi wanachama
f) Kuongeza ushindani wa biashara ya mbegu ndani na nje ya Tanzania
g) Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu na matumizi ya mbegu zenye ubora kwa nchi wanachama
h) Kuondoa vikwazo katika biashara ya mbegu kimataifa na kuhakikisha ufuatiliaji wa taarifa za kina za mbegu zinapatikana muda wowote.

➢ **Tanzania ni mwanachama wa "UPOV (International Union for Protection of New Varieties") Tangu mwaka 2015 Tanzania ilijiunga na UPOV**

**Faida za kujiunga na shirika hili kwa Taifa ni:**

a) Kusaidia upatikanaji wa aina mpya za mbegu za mazao kutoka nje na kuboresha programu mpya za ugunduzi wa mbegu
b) Kulinda haki miliki za wagunduzi wa mbegu hapa nchini na kusaidia wagunduzi kufikia mbegu za nje ya nchi
c) Kuongezeka kwa ugunduzi wa mbegu za mazao tofauti zilizoboreshwa zaidi
d) Kuongeza ushindani katika sekta ya mbegu na kuingia katika masoko ya nje ya nchi.

➢ **Kuboresha sheria na kanuni za mbegu katika eneo la Mashariki pamoja na eneo la Kusini mwa Afrika (SADC) ili kurahisisha biashara ya mbegu kati ya nchi washiriki**

**Faida za Uanachama wa Tanzania katika Jumuia za Kikanda hizo ni pamoja na:**

a) Itawezesha Tanzania kufanya biashara ya mbegu kimataifa kwa kuondoa vikwazo vya kitaalamu vinavyoweza kuzuia mbegu kutoka Tanzania kwenda nchi zingine. Hii inatokana na kutumia mifumo ya pamoja ya taratibu za uthibiti na udhibiti ubora wa mbegu. Tanzania kujiunga na mifumo huu wa uthibiti wa mbegu wa SADC na eneo la Mashariki mwa Afrika inahamasisha wazalishaji wa mbegu kuzalisha kwa wingi kwa kuwa mbegu itakayozalishwa na kuthibitishwa ubora wake kwa kuzingatia taratibu za Mashariki mwa Afrika na SADC itaweza kuuzwa kokote katika nchi wanachama.

**Faida za moja kwa moja ni kwamba:-**

- Itasaidia katika ongezeko la upatikanaji wa mbegu bora nchini hivyo kuongeza uzalishaji kwa wakulima,
- Kuongeza mapato ya fedha za kigeni kwa kuuza mbegu nyingi nje ya nchi,
- Ongezeko la ukusanyaji wa kodi kutokana na mauzo ya mbegu nchini,
- Upatikanaji wa ajira kwa Watanzania kupitia uzalishaji wa mbegu,
- Kupanda kwa thamani ya ardhi ya Tanzania kwa sababu itakuwa na uhitaji mkubwa katika uzal ishaji wa mbegu,
- Ongezeko la viwanda vya kuchakata mbegu za mazao hivyo kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati.

b) Mfumo wa SADC unaongeza uwazi. Hii ni kutokana na kwamba mfumo huu huweka wazi vigezo vya ubora wa mbegu vinavyokubalika kwa mbegu kuuzwa katika nchi wanachama. Aidha, aina za mazao zilizoidhinishwa kwa nchi mwanachama huorodheshwa kwenye orodha ya mbegu za SADC (SADC Variety Catalogue)
c) Inasaidia nchi kushiriki katika maamuzi ya kuandaa kanuni za kimataifa zinazosimamia ubora wa mbegu kwa kuweka makubaliano ya pamoja ya viwango vya ubora kwa jamii mbalimbali za mazao kwa nchi wanachama
d) Taifa linafaidika kwa kubadilishana uzoefu na taarifa na taasisi nyingine zinazohusika na uthibiti wa ubora wa mbegu pamoja na mashirika mengine ya kimataifa. Hii inajenga mahusiano mazuri kati ya Serikali na sekta binafsi.

**Faida ya Ithibati ya ISTA na Uanachama wa Skimu za Mbegu Za "OECD" pamoja na UPOV**

- Kwa kukamilisha matakwa na kwa mwanachama wa taasisi za kimataifa, uzalishaji wa mbegu hapa nchini utaongezeka kwa kuwa wafanyabiashara watakuwa na uhakika wa soko la mbegu zao ndani na nje ya nchi
- Ubora wa mbegu utaongezeka
- Bei za mbegu zitapungua

# Michezo

Ijumaa Oktoba 30, 2020

Nipashe



Messi ni 'Harry Potter' wa soka - Vieri UKURASA 20



Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (kushoto), akifunga bao la lake la kwanza na la pili kwa timu yake huku golikipa wa RB Leipzig, Peter Gulacsi akiruka bila mafanikio katika mechi ya Kundi H ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. United ilishinda mabao 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# Kaze afunguka Biashara haichomoki

## Kocha huyo aeleza ameandaa mfumo mpya utakaowamaliza katika mchezo wa ligi...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kinatarajia kwenda kutembelea kaburi la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere leo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze amesema malengo yake ni kuona timu hiyo inapata matokeo ya ushindi tu katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze, alisema kikosi chake kilichoweka kambi ya muda jijini, Mwanza, kiko tayari kwa ajili ya kuwakabili Biashara United na mikakati yake ni kuondoka na pointi tatu muhimu.**

Kaze alisema anajua mechi hiyo itakuwa na ushindani kutokana na rekodi nzuri ya Biashara United wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani na ubora wa kikosi cha wapinzani wao.

Mrundi huyo alisema wamefanya maandalizi mazuri na anaamini Yanga ina nafasi nzuri ya kushinda mchezo huo huku wachezaji wake wakionyesha ari na morali kubwa ya kupambana kutafuta matokeo mazuri.

"Hakuna mechi rahisi kwetu, kila mchezo ni fainali kwetu, tumejiandaa kutafuta pointi muhimu katika mechi hii ili tuendelee kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yetu tunayoyatarajia," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema kila mechi anaingia tofauti kwa sababu ya mfumo wanaotumia timu pinzani na kamwe Biashara United isitarajie kuiona Yanga waliyokutana nayo msimu uliopita au iliyocheza na KMC.

"Ninafanya mabadiliko ya mfumo kulingana na mpinzani ninayekutana naye, lakini nikiwa na lengo la kutafuta pointi tatu muhimu, tunahitaji kuendelea kupata ushindi mwingine nje ya uwanja wa nyumbani. Hii itatusaidia kufikia mipango ya klabu na timu kwa ujumla," Kaze alisema.

Aliongeza ataendelea kuwakosa wachezaji watatu ambao ni majeruhi na waliachwa Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

"Tutamkosa Carlinhos (Carlos), ambaye anatibiwa jeraha la enka, Balama Mapinduzi ambaye tatizo lake nimelikuta pamoja na Haruna Niyonzima anayesumbuliwa na malaria, hawa hawako kwenye mipango ya mechi ya Jumamosi," aliongeza Kaze.

Hata hivyo kocha huyo alisema kwake jambo muhimu ni kupata ushindi na suala la idadi ya mabao watakayofunga halimpi presha kwa sasa.

"Kwanza ninaangalia pointi tatu, mimi sijali tunapata idadi gani ya mabao, kikubwa tupate ushindi, tunaifuata Biashara United kwa ajili ya kuvuna pointi nyingine, hautakuwa mchezo rahisi kwa kila upande, sisi tunahitaji ushindi na wenzetu pia wataingia na mipango yao, tunapambana ili kufikia malengo," alisema kocha huyo.

Kaze ataiongoza Yanga kwa mara ya tatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini tayari ameshinda michezo miwili tangu alipotua klabuni hapo mapema mwezi huu.

# Morrison, Lawi rasmi kifungoni

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Bernard Morrison, amefungiwa kucheza mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara na kutakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 kutokana na kumpiga ngumi beki wa Ruvu Shooting, Juma Nyosso.

Morrison alitenda kosa hilo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa mapema wiki hii, ambayo ilimalizika kwa Simba kulala bao 1-0.

Taarifa ya Bodi ya Ligi Kuu Nchini (TPLB), imesema adhabu hiyo imetolewa kupitia kanuni ya 39 (5) ya Ligi Kuu inayokataza mchezaji kufanya kosa la kupiga.

Kwa adhabu hiyo, Morrison sasa atakosa mechi dhidi ya Mwadui FC itakayofanyika kesho, Kagera Sugar iliyopangwa kuchezwa Novemba 4, mwaka huu na dhidi ya watani zao Yanga inayotarajiwa kufanyika Novemba 7, mwaka huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa kutoka Ghana alionekana akimpiga ngumi Nyosso wakati wachezaji wa Ruvu Shooting wakigomea penalti iliyotolewa kwa wapinzani wao Simba katika mchezo huo.

Wakati huo huo, Gwambina FC imepigwa faini ya Sh. milioni tatu kwa kosa la kuvaa jezi ambazo hazina nembo ya mdhamini katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Pia mchezaji wa Polisi Tanzania, Daruwesh Saliboko, amefungiwa michezo mitatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000 baada ya kumpiga ngumi mchezaji wa Gwambina katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Tanzania Prisons yenyewe imetozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kuingiza magari ya viongozi na mashabiki wakati mchezo kati yake na Simba ukiwa unaendelea huku adhabu ya faini kama hiyo ikimkuta mchezaji wake, Salum Kimenya na kufungiwa miezi mitatu kwa kumpiga ngumi Morrison.

Pia bodi hiyo imemfungia mwamuzi, Shomary Lawi kuchezesha soka kwa mwaka mmoja kwa kushindwa kumudu mchezo huo uliochezwa Oktoba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >